SHALOM

Habari za asubuhi marafiki. Mwaweza kuketi chini. Ni vizuru kurudi upande wa nyuma wa jangwa. Wajua ah tunaamini wakati wa mwisho nilipokuwa humu, nalipaita mahali hapa, "upande wa nyuma wa jangwa." Hapo ndipo sisi kwa kawaida humpata ah Bwana ambapo alipatwa wakati mmoja na Musa alipokuwa akichunga kondoo upande wa nyuma wa jangwa.

Huyu mtu nilimwona kwa kioo cha kutazamia nyuma wakati mchache uliopita. Nilopkuwa nikija nilisikia hivi majuzi alikuwa hospitalini nami nilikuwa nikimwombea na ndiye huyu ameketi hapa ah [Mtu fulani kusanyikoni asema yeye ni mzima—Mh.] Loo, hilo ni njema. Nashukuru sana, yeye alikuwa akitokwa na damu nami nafurahi sana kumwona asubuhi ya leo.

Nina furaha kuu kumwona yeye asubuhi hii. Nasikitika kusikia kuhusu ndugu huyu aliyekuwa hapa pamoja nasi humu, aliye na ugonjwa wa kansa, hospitalini. Twajua kuwa tuna njia moja pekee iliyo kuu ya kutoka humu, na hiyo ni njia ya kifo. Yaani, yatupasa sote tupitie katika njia hiyo, hata kama tu wenye haki sana, watakatifu sana kati yetu, sisi hubebana sisi kwa sisi hadi kaburini mmoja kwa juu ya kaburi la mwingine. Na hali Yesu alisema, "Yeye aniaminiye hatakufa kamwe." Lakini kile yale "mauti" ilicho hapa, si kile tukiitacho kifo.

2 Kama wakati Yesu aliponena kuhusu Lazaro, Yeye alisema, "Yeye analala."

Na wakasema, "Vema, tuta. . .Hufanya vyema iwapo analala."

3 Ndipo Yesu alisema, ilimbidi awaambie katika lugha waliyoifahamu, mwaona, "Yeye amekufa." Yeye alisema, "Na kwa ajili yenu ninafurahi sikuwa hapo, lakini nitakwenda kumwamsha." Mwaona?

4 Na hapo ndipo Yeye aliponukuu maneno hayo ya ajabu tuliyo nayo Maandikoni, "Yeye asikiaye, yeye aniaminiye Mimi, yuna Uzima wa milele; hataingia hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani. Mimi ndimi huo ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Naye kila aishiye na kuniamini, hatakufa kabisa hata milele." Waona? Hatakufa kabisa: Hakuna . . .Hakuna mauti hasa kwa Mkristo.

Mauti maana yake ni "Kutengana milele."

5 Na sasa kama vile tulivyo. . .kufa, kama katika mwili wa kawaida jinsi tulivyo sasa, tunatengana mmoja na mwingine. Lakini, hasa mwili huu ndio unatutambulisha sisi kwa sisi kwa maana sisi hutegemea zile hisi tano: kuona, kuonja, kugusa,

kunusa na kusikia. Na mradi tu tuwezapo kuonana kwa macho na kugusana sisi kwa sisi, naam, tuna ushahidi kuwa sisi tuko hapa. Ikiwa u kipofu na huwezi, na—na huwezi kuona, basi waweza kumpapasa mwingine, nasi . . . au kumsikia mwingine. Nazo hisi za duniani hutambuana.

6 Lakini, hakika, kwa kweli, hatujawahi kuonana wenyewe kwa wenyewe. Je, ulijua hilo? Hatujaonana wenyewe kwa wenyewe. Wewe husikia kitu fulani kikinena toka mwilini humu kinachoiga cho chote kilicho ndani. Kwa hivyo basi tunapoongea sisi kwa sisi, sisi—sisi hatuuzungumzii hasa mwili huu. Ni ile roho iliyo ndani, lakini mwili ndio kitu kinachotambulisha ile roho iliyo ndani. Na kwa hivyo tunapoongea sisi kwa sisi, tuna . . . kwa upesi twaweza kufahamu mara moja ikiwa sisi tu Wakristo au la, kwa sababu kuna ushirika wa roho tunayoongea kutoka kwake. Mwaona, kuwa hutetemeka kama mawimbi hadi kwa mwingine kama tu Wakristo au la. Kwa hivyo hatujaonana wenyewe kwa wenyewe.

7 Yesu. "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; lakini Mwana pekee wa Baba ndiye aliyemufunua." Mwaona? Yaani, Mungu alidhihirishwa. Utu ule—ule wa Mungu ulidhihirishwa katika Mwili wa Bwana Yesu Kristo, kwa hivyo Yeye alikuwa amejionyesha kwa sura kamili ya Mungu. Au, Mungu alijieleza Mwenyewe katika sura, mwaona, katika sura, ya Mwanadamu, Mungu alijionyesha Mwenyewe kwetu na Yeye alikuwa Mungu. Si nafsi ya tatu au nafsi ya pili; Yeye alikuwa ndiye ile Nafsi, Mungu. Yeye alikuwa Mungu Mwenyewe, akijidhhirisha Mwenyewe, ili tumpapase Yeye.

8 1 Timotheo 3:16, "Na bila shaka, yaani ubishi, siri ya utauwa ni kuu, Mungu alidhihirishwa au akajulikana katika mwili." Si ajabu hiyo? Mungu! Nasi hatungemfahamu kamwe Mungu alipoenenda katika hiyo Nguzo ya Moto na kadhalika kama alivyofanya. Lakini twamfahamu Yeye awapo mmoja wetu, mwaona, Yeye awapo Mwanadamu. Ndipo Yeye angezungumza nasi, tungempapasa Yeye, kumshikashika Yeye, na kadhalika. Na kama Maandiko yasemavyo dhahiri kuwa "mikono yetu imempapasa Mungu," mwaona, kwa mikono yetu, kumgusa Yeye kwa mikono yetu.

9 Mungu yu katika mwanadamu. Naye anajijulisha Mwenyewe leo katika kanisa Lake. Katika Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, Mungu hujitambulisha Mwenyewe, kuwa Yeye hudumu Mungu. Na walimwengu watamjua tu Mungu wakimwona ndani yako na yangu. Hiyo tu ndiyo njia pekee watakayomjulia Mungu, ni sisi tukiwa barua zilizoandikwa, waraka wa Maandiko, tunasomwa na watu wote. Na maisha yale tunayoishi yaonyesha kile kilicho ndani yetu. Mtu hutambuliwa kwa matendo afanyayo. Kwa hivyo matendo yetu hayana budi kuwa mema, mwaona, kila mara mema kwa sababu tunamwakilisha Bwana Yesu Kristo.

10 Ni jambo la ajabu vipi hasa wakati m—mzee kama mimi husimama hapa na—na kuwaza kuhusu maisha haya yanayoelekea kwisha, yale yaliyopita, na—na nasi twaelekea katika hali ya usoni iliyo ya Milele. Na ningalijua kuwa maisha haya tu ndiyo niliyotumainia, ningekuwa mtu mwenye mashaka sana asubuhi hii. Lakini nijuapo kuwa maisha haya yamekuwa tu ki—kivuli cha yale ambayo ha—hayana budi kuja. Ni kivuli kwa sababu hayawezi kuwa kitu kamili kilichoumbwa na Mungu. Mungu haumbi cho chote kiangamiacho. Mwaona? Mungu ni wa milele. Na kwa hivyo, maisha haya tunayoishi sasa, yanaonyesha tu kile kilicho mbele yetu. Kile halisi kisichoweza kufa. Mwili ule usioweza kuangamia. Uzima ule ambao hauwezi kuchukuliwa. Mwaona? Na kwa hivyo Maandiko yako sahihi, yasemapo sisi tuna Uzima wa Milele, tuna Uzima wa Milele. Hatutakufa kamwe. Mwaona, kwa sababu unakuwa . . . Unapozaliwa mara ya pili unakuwa sehemu ya Mungu. Waona, wewe ni wa dawamu na Milele, hutashindwa. Wewe u sehemu ya Mungu, kwa sababu wewe u mwana Wake.

11 Sasa, naweza kuchukua jina lingine, na kusema jina langu ni fulani. Huenda nikachukua jina la mama yangu, Harvey, ambalo lingekuwa la karibu sana nami. Duniani, mama yangu alikuwa Harvey, na huenda naweza kuchukua jina la Harvey. Lakini bado tu damu itathibitisha kuwa mimi ni Branham. Waona? Kwa sababu mimi ni sehemu ya baba yangu. Na mradi tu ningali nina damu ndani yangu nitaendelea tu kuwa sehemu ya baba yangu. Waona, ndivyo. Na ninapozaliwa na Roho wa Mungu, Mimi ni sehemu ya Mungu, hivyo tu; na ninafanana Naye, waona, kuwa Yeye ni Baba yangu. Basi maisha yangu yapaswa yamwonyeshe Yeye; kama maisha yangu yamuonyeshavyo baba yangu wa duniani kwa ile sura aliyokuwa nayo. Wao husema mimi nimefanana sana na baba yangu, kwa hivyo basi ni sura yake inayoonyeshwa ndani yangu. Nayo ya baba yako imeonyeshwa ndani yako, na wazazi wako. Na kwa hivyo, Mungu Baba yetu huonyeshwa ndani yetu tunapozaliwa na—na kufananishwa hapa na sura Yake.

12 Sasa, naanza kunena, bado sijafikia somo langu juu ya kile nitakachowazungumzia.

13 Kila mara nimependelea mkutano ulio ndani ya nyumba, mkutano wa kibandani kama huu, zaidi ya—kuliko ninavyodhani watu wangedhani kuwa ningependa, kwa sababu mikutano bora sana na wakati mzuri sana wa ushirika ni kila mara katika mkutano wa maombi kibandani kama huu. Mahali ambapo nimesikia kuwa karibu sana na Mungu, ni wakati kundi dogo tu la waamini linapokutanika, na hapo twaabudu.

14 Sasa asubuhi hii, nadhani twaketi hapa watu thelathini, arobaini, thelathini, nadhani, au kiasi kama hicho, tukihesabu watoto. Singejua. Sijui sana ku—kuhesabu watu, natazama tu kundi dogo la watu, kwa sababu kuna vyumba vingine

hapa, mwaona, ambavyo siwezi kuwaona watu waliomo. Naam, lakini tunapokuja pamoja hivi najisikia ya kwamba tunakuwa pamoja sana kuliko tunavyoweza kuwa tuwako nje katika mkutano mkubwa, mno. Twaweza kunena wazi wazi. Na hiyo ndiyo sababu, asubuhi hii, nilidhani nikija hapa, kuwa ningezungumzia kusanyiko hapa asubuhi hii, pamoja na mchungaji wake mpendwa. Nina furaha kuwaona marafiki wengi wengi ndani humu, Strickers na wale wote a—ambao sijawaona kwa muda.

15 Nami ningewahubiria ninyi asubuhi hii Ujumbe wangu wa mwaka mpya niliokusudia kuunena Jumapili ijayo adhuhuri huko mkutanoni Phoenix, kwenye jumba la hotuba. Kwa sababu, ndani humu, nilidhani labda wananasia sauti kwa kanda hapa. Ambayo ni. . . Labda Roho Mtakatifu angenipa wazo bo—bora hapa kati ya kundi la waamini, kuliko pengine vile ingalikuwa huko Phoenix kati ya, mwajua, ambapo ni miongoni mwa kuamini na kutokuamini, na ushirikina na—na kila kitu vimechanganikana pamoja. Na ndipo ikiwa ndugu walikuwa wazitume kanda nje, hiyo ingekuwa—ingekuwa heri kufanya hivyo, kwa sababu ungepata kanda nzuri toka hapa. Niliwaambia vijana wachunguze vyombo vya kupasa sauti kwanza. Basi nilipokuja asubuhi hii, ndugu Terry aliniambia kuwa vyombo vya kupasa sauti ni vizuri. Kwa hivyo hilo—hilo ni njema. Kwa hivyo sasa hebu nasi kwanza, kabla hatujafikia jambo hili nzito, nami najua . . .

16 Naamini walisema wengine wenu mngebaki mpate chakula cha mchana, mtapata chakula cha mchana hapa bustanini au nyumbani, au popote pale mkiwa pamoja. Hilo ni njema sana. Mimi hufurahia nikiwaona nyote mkiwa pamoja.

17 Nami naona kuwa—kuwa Ujumbe wangu asubuhi hii unaelekezewa Kanisa la Mungu aishiye, mwaona, na ambalo naamini hii inayoketi hapa asubuhi hii ni sehemu yake. Na sasa kabla hatujafikia hiyo sehemu muhimu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mchache ili tuombe.

18 Baba yetu uliye Mbinguni, tuna shukurani sana Kwako, kuwa hata twaweza kuheshimiwa kukutaja Wewe kama Baba yetu, maana Baba yamaanisha kuwa tumezaliwa na Mungu mkuu aliyeumba Mbingu na Nchi. Nasi tuna furaha nyingi sana kwa ajili ya heshima hii, ambapo twaweza kuwaza mioyoni mwetu, na kuwa tu wana na binti Zako. Na halafu kukuona Wewe ukijitambulisha Mwenyewe kati yetu, kuwa Wewe u Baba yetu, ukigeuza mawazo yetu toka kwa mambo ya ulimwengu, na ukigeuza makusudi yetu na lengo na nia, na kila sehemu yetu, tukupende Wewe na kukuamini Wewe, na—na kujua kuwa ahadi zako ni za kweli.

19 Tumekusanyika hapa asubuhi hii mahali hapa tunapopaita "upande wa nyuma wa jangwa," au mimi ninapaita hivyo,

nikiwaza hivyo. Sababu niseme hayo, Bwana, si kuonyesha chochote juu ya kundi hili ndogo la watu, lakini, ni chochote kilicho cha hali dogo.

20 Lakini najaribu kuwaza kuwa ilikuwa Musa, mtumishi Wako, aliyekuwa upande wa nyuma wa jangwa, labda yeye pekee na kondoo zake na labda mkewe, Sipora, na—na—na Gershomu, mwanawe, huenda waliandamana naye. Mimi. . .Hiyo mimi sijui. Lakini huko ndiko walikuwa na tukio lililomgeuza nabii huyo, kutoka kwa mtoro mwoga hadi kwa Mtumishi wa Mungu aliyemwagiza kufanya kazi hiyo upande wa nyuma wa jangwa. Huko ndiko ambako—ambako hiyo Nguzo ya Moto iliyodhihirishwa kwa mara ya kwanza katika maisha ya mwanadamu, tujuavyo, moto huo ulikuwa huko katika kijiti kidogo jangwani, na hakikuteketea. Lakini—lakini ilikuwa ni ule Utukufu wa Mungu ukijionyesha Wenyewe katika kijiti hicho; ambapo Musa nabii alivua viatu vyake akakikaribia, na akaagizwa na Mungu kukomboa taifa la watu wa Mungu.

21 Na iwe hivyo tena leo, Bwana, upande wa nyuma wa jangwa ambako sasa twavua, tuseme, viatu vyetu, kofia zetu, na vyetu vyote, na kuviweka chini ya msalaba wa Kristo, na kusema, "Mimi hapa, Bwana, nitume."

22 Mbariki mchungaji huyu hapa, Ndugu yetu Isaacson, ndugu. Twaomba kuwa utambariki yeye na mke wake, na watoto wake; Ndugu Stricker, mkewe na watoto wake; na wengine wote waliowakilishwa hapa asubuhi hii.

23 Na tumekusanyika hapa; la, Bwana, si kwa utukufu mkuu, au tujulikane kama viongozi au—au baadhi ya. . . watu mashuhuri wa kitu fulani kikuu. Sisi tuna—tuko hapa tu kama waamini wanyenyekevu. Sisi tuko hapa kwa sababu twakupenda Wewe, nasi twapendana. Na tuonanapo na tunapokutana pamoja, twaona yaonekana dhahari kuwa Mungu ndiye amejikusanya pamoja wakati kila mwamini anajikusanya mwenyewe katika mahali fulani. Na Yesu alisema "Mkitenda haya katika Jina Langu, basi nitakuwa kati yenu!" Nasi twajua kuwa Wewe uko hapa.

24 Nena nasi, Bwana. Na ikiwa haya maandishi ya muhtasari niliyoyaandika hapa, na Maandiko ya kutumia, hayafai, asubuhi hii, kwa wazo ambalo ungetukubalia tuwaze, basi Bwana, tuliache hilo, na kutenda jinsi utuambiavyo tutende. Tubariki sasa, maana twaomba hili katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

25 Basi, katika kusoma Maandiko, ilikuwa kwamba nili. . . kabla sijawa na umri mwingi, ningekumbuka vema. Na siku hizo ninge. . .siku za ujana wangu, sikuhubiri ujumbe mrefu, labda dakika thelathini au muda wo wote kama huo, nilichambua katika wazo moja na kuliweka mawazoni. Lakini sasa ni. . .sababu ya kuwa na hii mikutano mirefu sasa, ni kwa sababu ninanasa kwenye kanda. Mwaona? Na kanda hii,

wale vijana hapo wanaponasa, wataanza wakati fulani, labda sasa, mwanzoni mwa maombi, na inatumwa kwingi, mahali pengi, kote ulimwenguni. Kwa hivyo tutanena asubuhi hii juu ya mwaka mpya. . . tunaouita Ujumbe wangu wa mwaka mpya. Nilijaribu, nikawa na jumbe tatu za Krismasi, nami najua ninyi watu nje hapa upande wa nyuma wa jangwa mnapata hizo kanda. Na juu ya-juu ya Ujumbe wangu wa mwisho huko kanisani, au uliofuatia ule Ujumbe wangu wa mwisho, ulikuwa juu ya *Ile Nuru*. Na ikiwa huna kanda hiyo, nina hakika utaufurahia sana. Niliufurahia Sana, ule upako wake, ambao Bwana alinipa.

26 Naam, leo tunapoelekea ya mwaka mpya, ni—ninataka kuwaza si kama wakati uliopita, lakini nataka kutazama ya usoni. Mwaona? Kama vile Paulo alivyosema, "Nikiyasahau yale yaliyo nyuma, nakaza mwendo, niifikilie mede ya dhawabu, mwaona, ya wito mkuu." Na kama inavyotajwa, ni kama kutazama nyuma katika kioo cha gari. Tunayatazama yale tumepita, tunapotazamia katika kioo cha kuangalia upande wa nyuma wa gari. Sasa hatutajaribu kuuweka Ujumbe wa leo kama kutazamia kwa kioo cha kuona nyuma. Ingechukua muda mrefu sana, mwaona, mambo, yale Bwana ametenda. Nanyi nyote mnafahamu yale mambo makuu ambayo Bwana amekuwa akitenda, ni baadhi ya mambo makuu sana niliyowahi kuona maishani mwangu, Yeye ya—yametokea tu katika miezi michache iliyopita. Na, ingawa sasa tuna shukrani sana kwa yale yamekuweko, lakini sasa tunatazama mbele. Tunatazama ambako tunakoelekea, na katika huu mwaka wa 1964.

27 Na sasa ikiwa ninyi hapa mwapenda kusoma, au—au ningependa kusoma baadhi ya Maandiko, kwa sababu hili lote lina msingi juu ya Neno Takatifu la Mungu.

28 Na yaniachia sasa karibu saa moja na dakika kumi na tano, kwa ajili ya kanda hii. Na, Bwana akipenda, nitajaribu kuumaliza ili mwende kula chakula cha juoni. Nawashukuru kwa kuniambia kwamba nilikuwa na wakati hadi saa kumi na mbili jioni. Hilo lilikuwa njema sana.

29 Sasa na tufungue katika Biblia mahali pawili, vitabu vinavyokaribiana sana. Ni katika Agano la Kale. Nachukua fungu nitakalosoma, toka mahali pawili, Isaya 62 na Zaburi 60. Sasa katika Isaya 62, tutafungua tusome kwanza. Na katika haya, tumekumbushwa kuhusu nguvu kuu za Bwana Mungu wetu, na jinsi—jinsi Yeye alivyo mkuu, na jinsi Mungu wetu alivyo mwenye enzi. Nasikitika ni Isaya 60 badala ya 62, Isaya 60. Vema, basi twasoma haya, Isaya 60:1 na 2.

> *Ondoka uangaze; kwa kuwa nuru yako imekufa. Na utukufu wa BWANA umekuzukia.*

Maana. . .tazama, giza litaifunika dunia. Na giza litazifunika kabila za watu; Bali BWANA atakuzukia wewe. Na utukufu wake utaonekana juu yako.

30 "Giza kuu litazifunika kabila za watu." Huu hakika, huu ni unabii wa siku tunazoishi sasa.

31 Sasa na tufungue Zaburi. Naanini kuwa labda nimechanganyikiwa ambapo nimeandika Maandiko hapa, nilipokuwa na haraka usiku uliopita katika kuyaandika, kuyaandika haya. Zaburi 62:1 hadi 8.

Nafsi yangu yamngoja Mungu peke yake kwa kimya, wokovu wangu hutoka kwake.

Yeye tu ndiye mwamba wangu na wokovu wangu, Ngome yangu, sitatikisika sana.

Hata lini mtamshambulia mtu, mpate kumwua ninyi nyote pamoja? Kama ukuta unaoinama, kama kitalu kilicho tayari kuanguka.

Hufanya shauri kumwangusha tu katika cheo chake; Huufurahia uongo. Kwa kinywa chao hubariki; Kwa moyo wao hulaani.

Nafsi yangu umngoje Mungu peke yake kwa kimya. Tumaini langu hutoka kwake.

Yeye tu ndiye mwamba wangu na wokovu wangu, Ngome yangu, sitatikisika sana.

Kwa Mungu wokovu wangu, na utukufu wangu; Mwamba wa nguvu zangu, na kimbilio langu ni kwa Mungu.

Enyi watu, mtumainini siku zote, ifunueni mioyo yenu mbele zake: Mungu ndiye kimbilio letu.

32 Sasa, ikiwa ulichunguza katika kusoma Maandiko hapa katika Zaburi, ilizidi kusema, "Mungu ndiye mwamba wangu." Je, wajua mwamba unawakilisha nini katika Biblia? Mwamba katika Biblia, hapa, huwakilisha "ufunuo wa Mungu." Waona, "Mungu ndiye ufunuo wangu." Yeye ndiye, unaona. Ule ufunuo wa Neno ni mwamba.

33 Sababu, siku moja Petro alipo. . .Yesu alikuwa ameuliza swali, "Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?

34 Na mmoja wao alisema, "Wewe u. . .Wengine husema Wewe u Musa, au Eliya, Yeremia, au mmojawapo wa manabii." Lakini swali halikuwa hilo.

"Nanyi mwaninena kuwa ni nani?

35 Yeye, Petro alisema, maneno haya mashuhiri sana, na kusema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

36 Yeye alisema "Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni. Na juu ya mwamba huu!" Mwaona?

37 Na Daudi akinena hapa, "Mungu ni mwamba wetu." Mungu ni mwamba wetu Mungu wakati afunuliwapo kwetu. Huo huwa mwamba, mwaona, Mungu yu mwamba wetu.

38 Sasa somo langu la asubuhi hii ni neno geni: *Shalom*. *Shalom* katika Kiebrania maana yake ni "amani." Na hilo ndilo ninaloambia Kanisa asubuhi hii, "Shalom!" Hiyo ni amani.

39 Katika Kifinishi inaitwa *Jumalan rauha*, ambayo yamaanisha "amani ya Mungu" juu yenu. *Rauha*. Mungu, mwaona, amani ya Mungu, Shalom.

40 Ujumbe wangu wa mwaka-mpya ni kwa kanisa lililoteuliwa katika Yesu Kristo kwa mwaka 1964. Si—si tu kundi la makanisa; bali Mteule, yule Bibi, Bibi wa—wa Kanisa. Bibi-arusi wa Kristo, mwaona, huyo ndiye ninayemzungumzia.

41 Tunakabiliana hapa, katika masomo yetu mawili tuliyoyasoma, vile vifungu viwili, namaanisha, kinyume kabisa cha moja kwa nyingine. Katika Isaya, yasema, "Ondoka uangaze, kwa kuwa nuru yako imekuja. Nuru ile iko hapa. Ndiposa katika kifungu kinachofuata, yeye asema, "Giza kuu litazifunika kabila za watu." Na ndipo tuko katika machanganyiko wa Nuru na giza, na hotuba yangu kwa Kanisa ni "Shalom, amani," na tuone haya yote ni nini, mwaona. Tunaukabili mwaka huu, tukiwa na zote mbili giza na Nuru. Tuna. . .ulimwengu uko katika mojawapo wa nyakati za mchafuko zaidi wa giza ambao umewahi kuwa ndani yake; hata hivyo umesimama, tena, ndani ya Nuru iliyobarikiwa sana iliowahi kuuangazia. Na kuna . . .

42 Tofauti tu ni kama ilivyokuwa mwanzoni, wakati kulikuwako giza kuu duniani. Na Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji na kusema, "Iwe nuru." Na Mungu akatenganisha nuru na giza. Nami naamini kuwa sasa tunaishi katika saa hiyo tena, ambapo Mungu anatenga Nuru na giza, na Yeye anaisukumia upande mwingine wa duniani ili Nuru iweze kudhihirishwa. Na sisi tuna . . .

43 Basi, lile—lile Kanisa, kusudi la kusema, "Shalom" kwao, ni kwa sababu hiyo ni Amani ya Mungu. Hilo ndilo ninalotaka kuwaletea asubuhi hii, kwa mwaka mpya, si kutazama nyuma, lakini tunatazama mbele hata kupambazuka kwa siku mpya. Hadi, kuna kitu fulani kikuu kilicho mbele yetu, ambapo miaka imekuwa na furaha tuliyotazamia, kuomba sana, kuja kwa ile Nuru kuu. Na sasa twaweza kuiona ikipambazuka huko kwenye upeo wa macho, mazingara ya upeoni, ni kupambazuka kati ya kuharibika na kutokuharibika. Twaona ikipambazuka kati ya mbingu na nchi, kutoka kwa magonjwa na taabu za dunia hii, hadi kwa siku inayong'aa ya Uzima wa milele na mwili usioharibika na dunia isiyoharibika ambayo haitapita kamwe.

Hiyo—Hiyo ni "Shalom," kwa—kwa Kanisa. Sasa, ni wakati wa Nuru unaokuja kwa waamini, lakini giza kuu kwa watu. Mimi. . .

44 Hivi majuzi tulikuwa tukiongea mimi na mke wangu, na tulikuwa tukiongea kuhusu ile—ile saa tunayoishi. Naam, sababu ya kupachagua mahali hapa, nilijisikia tu kama kutokuzuia chochote na kuongea nanyi, mwaona. Mwaona? Hivi ni inaonekana kama kwamba kuna wakati ulio juu ya watu ambao ni wakati wa huzuni sana ninaoweza kuukumbuka.

45 Nimejaribu kila mara kadiri niwezavyo, katika kutokubishana na watu katika mambo ya kidini; lakini ikiwa singeweza kumsalimia kwa mkono baadaye, haijalishi lingekuwa jambo kali vipi, na kumsalimia kwa mkono, na kusema, "hii ni katika nuru ya kuelewana vema kati yetu," nami ningali nampenda mtu huyo (si kusema tu kwa kinywa changu, lakini kwa moyo wangu), ndipo si—sipaswiwa kwenda nje huko na kujaribu kuzungumza na watu. Kwa sababu, mwaona, lazima tutende hivyo, lazima tumpende mtu huyo. Mwaona? Na kuendelea kati ya watu wa kila tabaka, na madhehebu na makabila mbalimbali, na dini na kadhalika, na kujaribu kuiweka Biblia chini, na kusema, "hebu—hebu na tujadiliane si kwa kanuni zako za imani wala kwa vitabu vyenu vya elimu ya maadili, bali kwa Biblia." Na ndipo siyo. . .Labda wakati mwingine mtu hunena kwa ukali sana; lakini ikiwa nina wazo moja kuwa sikumpenda mtu huyo, basi—basi najua jambo moja, Roho wa Kristo ameondoka kwangu. Ikiwa ni—ikiwa naweza kujisikia kuwa simpendi mtu huyo, kuna kasoro kwangu.

46 Kwa sababu Roho wa Kristo, wakati wao. . .ile. . . katika—katika kumsulubisha Yeye, na watu Wake Mwenyewe wakimpigilia misumari, na—na viumbe wale aliowaumba wakimpigilia misumari, wale Yeye aliwaumba wakiirudisha ndani ya mwili Wake wa kibinadamu. Walakini, akiwa na moyo uliojaa huruma, Yeye alilia, "Baba uwasemehe, hawajui watendalo," mwaona.

47 Na ni—nimefikia mahali hapo. Naamini kuwa watu hawajui watendalo. Inafikia wakati ambapo mwanadamu ana, anaonekana kama, anayetumikia maovu hadi ni—ni jambo la kuhuzunisha. Yaonekana kama kwamba ku—kuna uvuli wa giza juu ya watu, unaowagandamiza.

48 Kama, kwa mfano, jambo hili moja. Nimezuru mataifa na kunena, huku Bwana Mungu akilitambulisha, a—akibithibitisha Neno Lake na kuonyesha kuwa ni la kweli, na bila kuruhusu cho chote kinenwe bila kukitimiza hasa vile Yeye alivyokisema, akikinena na kuwepo, na mengineyo, kama vile Yeye amekuwa akitenda. Na watu huketi na kutazama hayo, na kuendelea katika h49i yao ile ile. Mwaona?

49 Mwaona, si kuwadharau kamwe, lakini kama dada zetu, mara nyingi nimewaambia kuhusu kuvaa mavazi hayo, na kukata nywele na mambo madogo madogo. Na, wanaume jinsi watakavyoendelea katika kanuni za imani zao, na—na kutumika katika hizo kanuni za imani na kadhalika. Na—na wao ni watu wazuri. Wao ni watu wema. Lakini yaonekana kuwa wao—wao—wao hawawezi kuelewa, yaonekana kuwa hawawezi kufahamu. Kwani? Narudi huko mwaka ufuatao, na badala ya kuwa bora, ni wabaya zaidi. Ina—inaendelea mbele. Hapa kuna dada ambaye kwa wakati mmoja alikuwa na nywele ndefu nzuri za kupendeza, naye amezikata. Hapa kuna mwanamume aliyeonekana kwa wakati mmoja kama aliyechukua msimamo wake na kuendeleza yaliyo mema; naye amerudia tena ile . . . kama mbwa arudiavyo matapiko yake, na—na nguruwe kugaa-gaa matopeni. Mwaona, anarudi tena katika hayo. Yaonekana kama kuna kitu fulani kilichowapata watu wetu, kilichoupata ulimwengu, kwa kuwa waonekana kwamba hawana ufahamu, kuna kitu fulani kasoro.

50 Kama tu vile uwaonavyo wanaume siku hizi, hupati ule wema katika wanaume. Huupati katika wanawake. Sasa, sineni kuhusu . . . Sababu ya kuweka msingi huu, ni kufikia "Shalom." Mwaona?

51 Lakini mwawaona wanawake katika siku zetu, waonekana kama hawana huo ubibi waliokuwa nao wakati mmoja. Wako tu kama wao—wao wanataka kufanya hivyo, lakini kuna kitu fulani kisichowaruhusu kutenda hivyo. Yaonekana kuna ugumu. Ati, unamwambia m—mwanamke kuwa haimpasi kutenda kitu *fulani na fulani* na yule mwanamke anakitazama Hicho na kukiamini Hicho, yeye anataka kukiamini Hicho, lakini kuna kitu fulani kinachomsukumia njia nyingine. Waona? Maskini yule, na—na namsikitikia. Yeye amenaswa sana kwa utando wa Hollywood na matangazo ya televisheni, redio, magazeti, kwenye barabara za mji, katika—katika madirisha ya maduka makubwa, na nguo za kisasa na mengineyo, na jinsi wanawake wengine wamkutavyo. Na inaonekana kuwa kuna jambo fulani ambalo hawawezi kujiambua kwalo; vijana wetu, wazee wetu, watu wetu wa makamu.

52 Inaonekana kuna kitu fulani katika mwanamume. Mwanamume haonekani kuwa, ana ule uanaume aliokuwa nao. Wanawake hawaonekani wana uanauke waliokuwa nao. Mchukue mwanamume wa siku hizi, wanaume hawaonekani shupavu kama walivyokuwa. Yote ni aina ya . . . Wao wanataka kuvaa viatu vya rangi ya zambarau, na—na wanataka kutenda kama wanawake. Naam, ndivyo. Kwa kadiri, yaonekana kama upotovu. Mwanamke ataka kukata nywele zake na kutenda kama mwanamume. Na mwanamume ataka kutenda kama mwanamke. Mwaona? Na hali unaweza kuwazungumzia, nao ni watu wazuri ukiwazungumzia, watu wazuri, wa kirafiki, hupenda maongezi. Nini kilisababisha haya? Ni

Giza hilo kuu juu ya watu, ni kitu fulani ambacho—ambacho kimewagandamiza kwake.

53 Kama Wayahudi walivyokuwa katika siku zile Yesu alikuja duniani, Isaya alikuwa ametabiri kuhusu hilo na kusema, "Kungekuwa na, wangekuwa na macho bali hawangeona na masikio na hawangesikia." Na hiyo ndiyo sababu Yesu aliwaombea msamaha, kwa sababu alibidi iwe hivyo kutimiza Maandiko.

54 Na imerudi tena kwetu. Biblia imenena kuhusu hayo siku hizi tunazoishi, na kusema mambo haya yangekuja, "giza kuu juu ya watu." Nasi twaliona, ila kuna kitu fulani ambacho tu, kwa udhahiri, watu wataka kutenda wasiweze.

55 Nikodemo alikieleza wakati mmoja mbele za Bwana, "Rabi, twajua kuwa Wewe u Mwalimu uliyekuja toka kwa Mungu, maana hakuna mtu angetenda mambo haya utendayo Mungu asipokuwa naye." Lakini ilikuwa ni giza hilo, au upofu, juu ya taifa la Kiyahudi, ili Masihi aweze kuja kumchukua Bibi—arusi kutoka kwa Mataifa. Iliwabidi wao wamkatae Yeye.

56 Na hilo ndilo giza kuu lililo juu ya makanisa na mengineyo siku hizi, kukosa kuona ile Nuru inayong'aa. Mwaona? Mwaona, inaonekana kuna ugandamizi mzito. Tuchukue baadhi ya wainjilisti wanaojulikana sana siku hizi, wao kila mara wanalilia mkutano wa ufufuo, na wanatenda moja kwa moja kuupinga; mwaona, pasipo ufahamu, bila kuelewa.

57 Nami sisemi hayo kwa—nikiwa na nia ya kujaribu kusema, "Sasa tumekwisha ona haya, na, 'utukufu kwa Mungu' wao—wao hawamo ndani yake." Sijaribu ku—kusema ya kwamba katika. . .kuwafanya watu wadhani, "Vema, Ndugu Branham, ndiwe—ndiwe tu pekee uliye na ile kweli iliyoko duniani." La, hili ni kosa. Mwaona?

58 Ninasema hayo tu kulingana na ile Nuru ya saa tunayoenenda ndani yake, na kwa manufaa ya watu wale wanaojaribu kutafuta Nuru hii. Hakika, Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kunijia Mimi asipovutwa na Baba Yangu." Hakuna mtu atakayewahi kuiona. Ni ule Uzao uliochaguliwa awali, na huo pekee ndio utaipokea. Lakini tumefikia tena mahali hapo tena. Biblia ilisema kuwa, "Ninyi ni nuru ya ulimwengu."

59 Nabii alisema, "Giza kuu litazifunika kabila za watu," kufunika watu wa ulimwengu kwa wakati huu. Na hilo hasa ndilo tulilo nalo, giza kuu limefunika watu wa makabila yote.

60 Mungu katika rehema Yake kuu, kama vile nimehubiri kila siku na kushikilia, kuwa Yeye kila mara huonyesha vituko Vya—Vyake toka mbinguni, vituko Vyake vikuu vilivyo muhimu, hutendeka mbinguni kabla havijatendeka duniani. Yeye hujionyesha Mwenyewe. Kwa maneno mengine, kabla Masihi hajafikia mahali ambapo huduma Yake ingeanzia, palitokea Nyo—Nyota toka Mbinguni iliyowaongoza hao watu hadi ma—

ma—mahali alipokuwepo, wale mamajusi. Kama mlivyosikia katika Ujumbe wangu uliopita jinsi Mungu alivyowafanyia wa—wale mamajusi, na—na katika siku ambayo Yeye aliwafanya kwenda upande mwingine kwa ndoto, kisha akamwambia Yusufu kwa ndoto kuhusu utunzaji wa Mwanawe. Kwa sababu yeye alipata ndoto, kulikuwa na . . .

61 Ndoto ni kitu cha pili, kitu kisicho bora sana, kwa sababu watu wanaweza kuwa na ndoto zisizo kweli. Lakini hapakuwepo nabii nchini siku hiyo, ona, hapakuwako nabii, kwa hivyo ilimpasa Mungu kutumia kile alichokuwa nacho. Basi inatufunza kuwa—kuwa Mungu aweza kutumia kila sahemu na kila kitu tutendacho, ikiwa kimewekwa wakfu Kwake. Lakini kwanza lazima kiwekwe wakfu Kwake. Hebuni ku—kumwazieni Mungu kwenu ambako hasa huonyesha ndoto zenu, mwaona, kwa sababu ni akili zifanyazo kazi ukilala. Ukichunguza ndoto, utaona kuwa ni jambo fulani ambalo wewe umekuwa ukiliwazia au kitu kama hicho. Kwa kawaida, mnaona. Na mawazo yenu yawe juu ya Mungu basi, mwaona, yaonyeshe jambo fulani kumhusu. Na cho chote ulicho, na kimwonyeshe Yeye.

62 Sasa, katika mbingu za juu. Je, ulitambua ninatazama hii, ile—ile Nuru kwenye ile picha hapo katika gazeti la Life, ambalo ndugu anayeishi hapa nyumbani ameiweka ukutani mwake, hiyo Nuru yenye pembe tatu.

63 Nimeikumbuka sasa hivi. Ikiwa ye yote wenu ana nakala ya tafsiri ya Lamsa ya Biblia, ukichungaza juu ya jalada lake, kuna utatu, nuru yenye ncha tatu, kama duara ya mwangaza. Na wakati Dr. Lamsa, rafiki, rafiki yangu, alikuwa akifasiri Biblia, huo ni mfano wa kale wa Kiebrania wa Mungu katika njia ya utatu halisi Yeye alivyo; si Miungu watatu, lakini madihirisho matatu ya Mungu yule: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ile Nuru ni Nuru duara nzima ya Nuru katika umbo la pembe tatu, ambazo zamaanisha kwamba Mungu atakaa katika afisi tatu, Ubaba, Uwana na wakati wa Roho Mtakatifu, yote Mungu yule yule.

64 Lakini, je, ulitambua kabla zile Mihuri Saba kufunuliwa, kabla ya Nuru kuu ya ajabu kujitokeza mbinguni juu papa hapa juu ya Tucson, Flagstaff, tulipokuwa? Ndugu Fred, wale wanaume wawili waliokuwa . . . wale wanaume wawili walikuwa pamoja nami asubuhi hiyo. Naam, hilo lilikuwa limeelezwa miezi na miezi hapo kabla, kuwa lingetendeka. Ndugu Fred Sothmann na Ndugu Gene Norman pia wanaoketi hapa asubuhi hii, wakati ili . . . walikuwa pale mlipuko ule ulipotokea, na sikujua haya yangetendeka. Naye alinituma nirudi, alisema ya kuwa wakati u karibu kwa ajili ya zile Mihuri saba zilizoshikilia zile siri saba za Biblia nzima, ilitiwa muhuri kwa zile Mihuri Saba. Na jinsi malaika hawa njiani kote, wale wajumbe wa zile Nyakati za Kanisa, walivyofungua sehemu fulani ya hizo. Lakini katika wakati wa saba, yule mjumbe wa saba, siri hizi zote

hazina budi kutimizwa. Mwaona? Yule mjumbe wa saba aliye wa duniani, waona, malaika huyu ambaye Yeye anena kumhusu wakati huo alikuwa duniani. *Malaika* maana yake ni "Mjumbe." Ndiposa, baada ya hayo, alimwona Malaika mwingine akishuka, si yule malaika aliye wa duniani aliyekuwa amepewa Ujumbe ule hapa, lakini yule (mwingine) Malaika mwenye nguvu akishuka kutoka Mbinguni akiwa na upinde wa mvua juu Yake, na akaweka mguu Wake juu ya nchi na juu ya bahari, na akaapa na Yeye aliye hai hata milele na milele, "Hakutakuwa na wakati tena baada ya haya." Mwaona? Lakini kabla Yeye hajavunja hizo Mihuri Saba kuzifunua, Yeye alizionyesha kimiujiza, Yeye alizionyesha kwanza huko mbinguni.

65 Siku hiyo walipiga picha kote kusini mwa Amerika na Mexico. Inaning'inia hapa katika gazeti liitwalo Life, ingali ni siri kwao. Lakini Yeye huitangaza mbinguni kabla hajatenda duniani. Yeye kila mara hufanya hivyo. Huonyesha ishara mbinguni kwanza.

66 Na hata katika yale Mafungu kumi na mawili ya Nyota. Sitarudi nyuma huko nifundishe alama za Nyota, lakini ninawaeleza ninyi tu kwamba mbingu hutangaza. Katika Mafungu ya Nyota twaona, katika lile kundi la Nyota, kuwa Yeye alieleza Biblia yote katika Mafungu ya—ya Nyota. Twaona kuwa Yeye huanzia, lile umbo la—la kwanza katika Nyota zile ni Bikira, na umbo la mwisho katika Nyota ni Leo Simba; ikionyesha kuwa Yesu angekuja duniani kwanza kwa Bikira, Yeye atarudi mara ya pili kama Simba wa kabila la Yuda. Mnaona? Yeye hupitia kwenye samaki waliokingamana kabla tu ya hayo. Wakati wa jamii ya Nyota iitwayo Kaa ndio tunaoishi sasa. "Na mbingu zote zamtangaza Yeye," Biblia ilisema hivyo.

67 Sasa, miezi michache iliyopita nilihubiri, kwa mfululizo wa mikutano huko kwenye Maskani, kuhusu zile *Nyakati Saba za Kanisa*. Ninyi, labda, nyote mmezisikia. Na nilipomaliza kuchora ubaoni zile Nyakati Saba za Kanisa, jinsi hiyo Nuru ilivyoingia na jinsi ilivyotoka. Nami nadhani mna hiyo, labda, mahali fulani hapa; lakini i kati yetu, kwa vyo vyote, twajua. Na ajabu ni kwamba, siku ya mwisho wakati ule Wakati wa mwisho wa Kanisa ulipochorwa, hii Nguzo kuu ya Moto (iliyo kati yetu) ilishuka chini kati ya mamia ya watu, na ikajirudisha Yenyewe nyuma hadi ukuta wa nyuma wa lile Jengo la ibada. Na hapo, mbele ya hawa mamia, ikazichora hizo Nyakati za Kanisa, ikiweka weusi na nuru, kama tu vile nilivyokuwa nimechora ubaoni. Kiajabu!

68 Sasa, majuzi, tumesikia kuhusu matukio ya historia ya kanisa sasa. . .Katika Bi—Biblia, *mwezi* huwakilisha "kanisa," na *jua* huwakilisha "Kristo." Maana twaona kuwa katika Ufunuo, sura ya 12, yule *mwanamke* aliyekuwa "kanisa," alionekana akiwa na mwezi chini ya miguu yake na jua kichwani mwake, nyota kumi na mbili kwenye taji yake. Ambapo, zile—

zile sheria za Kidesturi za kale za Kiyahudi zilikuwa chini ya miguu yake, na yeye alikuwa amevuka hizo akaingia kwenye nuru ya jua. *Nyota kumi na mbili* ni "wale mitume kumi na wawili" walioleta ujumbe kwetu, sasa, chini ya Roho Mtakatifu. Sasa twaona kuwa ule mwezi ulio angani huonyesha ile nuru ya jua, jua lisipokuwepo. Unatupa sisi—unatupa sisi nuru ya kutembea. Lakini bado ni . . . Haijalishi unaonyesha vipi, ingali bado si ile nuru halisi hasa, kwa maana unaonyesha. Na jua hung'aa kuelekea mwezi, nao mwezi huonyesha nuru yake jua lisipokuwepo. Lakini jua linapochomoza, basi mwezi hauhitajiki tena.

69 Na leo Kanisa linaonyesha Nuru ya Mwana wa Mungu asiyeko. Kanisa ni onyesho la ile Nuru. Kwa sababu Yeye alisema, "Kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena. Bali ninyi mtaniona Mimi, maana nitakuwa pamoja nanyi, na ndani yenu, hata ukamilifu wa wakati. Kazi nizifanyazo," Nuru zile Yeye alizozidhihirisha. Na hakuna Nuru ila kupitia kwa Neno la Mungu. Kulikuwa na . . .

70 Jua hilo ni Neno la Mungu. Hapo mwanzo, Mungu alisema, "Iwe nuru." Na wakati Neno la Mungu lililodhihirishwa, wakati Neno la Mungu lilipodhihirishwa, ikawa nuru. Kwanza, Mungu alilinena. Vipi kama halikudhihirishwa? Basi nuru haingekuwako bado. Lakini Yeye alipolinena, ndipo likadhihirishwa, likathibitishwa, Neno Lake lilidhibitishwa, nuru ikatokea.

71 Na hiyo ndiyo njia pekee inavyoweza kutendwa sasa, ni wakati Neno linapothibitishwa, lile Neno lililoandikwa la Mungu li—likithibitishwa, ndipo laonyesha Nuru. Ni, sehemu inawashwa, au inatolewa kwa kila wakati. Twaipata katika zile Nyakati za Kanisa, twaipata katika Nyakati za Kanisa la Agano la—la Kale. Kila wakati ilipofikia wakati wa dhihirisho fulani la safari, kulikuwa na nabii aliyekuja duniani. Na hilo Neno lilimjia nabii, naye akalifanya Neno hilo hai na Neno hilo lilipotambulishwa, lilimfunua Mungu. Ndipo wakati ukaanza, ikawa Nuru. Na hivyo ndivyo Nuru inavyokuja leo.

72 Sasa, sina chochote dhidi ya dhehebu lo lote, watu. Lakini nina yote niwezayo kuyawaza kupinga mipango hiyo kwa sababu imekosea. Na mpango wa kwanza uliowahi kuundwa ulikuwa ule—ule mpango wa Kirumi wa Kanisa Katoliki la Kirumi. Hilo ndilo lilikuwa dhehebu la kwanza lililowahi kuundwa, lilikuwa kanisa Katoliki la Kirumi, Nikea Roma. Yapata miaka mia tatu na ishirini na mitano baada ya kifo cha Kristo, 325, likajitokeza dhehebu la kanisa la Kirumi lililowaunganisha watu pamoja na kutupilia mbali chochote kilicholipinga. Hapo ndipo walipopata hayo mafundisho yao ya kigeni na kuanzilisha mpango ulio mbali na Neno. Na sasa kanisa hilo, tangu wakati huo, linaonyesha giza hasa, kwa sababu wakati huo twapitia kwa kile tunachokiita, "Zile

Nyakati za Giza," za miaka ipatayo elfu moja. Inajulikana kwa wanahistoria wote na wanavyuoni wa Biblia, na wengineo, kama Nyakati za Giza, ni wakati lile kanisa la Kirumi liliposimamia kila kitu.

73 Na kanisa hili la Kirumi ndilo "ma—mama wa makahaba," Biblia ilisema, katika Ufunuo 17, "yeye alikuwa kahaba, na mama wa makahaba. Naam, hiyo ni zinaa, mwanamke kuishi maisha maovu. Yote mawili ni jambo lile lile, yote ni sawa. Kwa hivyo kama—kama ni kahaba, hapana budi ni mwanamke. Kwa hivyo basi unaona kwamba si kahaba, bali "makahaba." Mwaona? Yeye ni "mwanamke," umoja, "kahaba." Kisha makanisa yanaitwa "makahaba," binti wa kahaba wa Kirumi. Yeye ndiye mama wa hao wote, mama wa madhehebu.

74 Na si ni jambo la ajabu, kuwa katika siku hii baada ya sisi kupitia katika mambo haya yote, na huu Ujumbe umetapakaa duniani ukipinga madhehebu, ukayalipua kutoka kulia hadi kushoto, kwamba, katika saa hii ambayo imenenwa tangu mwaka wa 1933, Roho Mtakatifu aliponipa maono haya na kunionyesha ule wakati wa mwisho, mambo saba niliyonena, na matano kati yao yamekwisha kutimia, kikamilifu, moja kwa moja, kama Ujerumani na—na Italia na vita hivyo vyote, na mambo ya mataifa (ni mara chache sana ambapo Yeye hunizungumzia mambo hayo). Lakini hayo yalitendeka hasa jinsi Yeye alivyosema yangetendeka. Jinsi Musolini angevamia Ethiopia, nayo Ethiopia ingeshindwa kwa urahisi, kisha jinsi angetahayarishwa, na kutemewa mate na watu wake mwenyewe; na kutahayarishwa na kuangikwa kichwa chini, pamoja na yule kahaba aliyeishi naye, kwenye barabara za mji. Jinsi Waamerika wingepigana vita na Ujerumani, wangepigwa sana mahali paitwapo, kituo kikuu cha askari ambapo pangekuwa na ngome ya saruji humo, naamini panaitwa Kituo cha Siegfried. Na kuna kingine kiitwacho Maginot, naamini kuwa hicho kilikuwa cha Wafaransa. Sivyo? Kituo cha Siegfried kilikuwa ni kituo cha Wajerumani. Na Bwana aliniwezesha nikione, miaka kumi na mmoja kabla hakijajengwa. Na wao hawangekubali kushindwa huko, Waamerika hawangekubali, hadi karibu waangamize jeshi lote. Wao walipoingia humo ndani wale Wajerumani walikuwa wameelekeza bunduki kwenye kikosi hicho, na kuwaacha waingie humo, nusura wakiangamize. Na niliona hilo, miaka kumi na mmoja kabla ngome hiyo hata haija—haijapata kuwekwa msingi, wala chochote kile, ile Ngome iitwayo Kituo cha Siegfried. Na mambo haya mengineyo, kama machine na magari, na—na jinsi kila kitu kimetendeka kama alivyosema, hata mwanamke kutawala taifa hili, ambalo, labda, ni kanisa. Kisha mwisho utakuja.

75 Sasa twaona kuwa katika mambo haya, mambo haya yote na jinsi nimeshambulia madhehebu, si ni ajabu kwamba papa wa Rumi angeondoka Rumi kwa mara yake ya kwanza kurudi tena

Yerusalemu? Na kwa kufanya hili. . .Jerusalemu imejulikana kama kanisa la kale sana ulimwenguni kote.

76 Melekisedeki alipokutana na Ibrahimu akitoka kupigana na wale wafalme, yeye alikuwa Mfalme wa Yerusalemu, Kuhani, ambaye alikuwa Kristo, alikuwa ni Mungu; hakuna mwingine yeyote angekuwa Melekisedeki ila Kristo Mwenyewe, Mungu Mwenyewe, mwaona, Mungu Mwenyewe, kwa sababu yeye hana baba wala mama, mwaona? Yesu alikuwa na baba na mama, mwaona. Kwa hivyo Mtu huyu hana baba, hana mama, hana mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa uhai Wake. Na hata awe nani, Yeye yungali hai. Na Yeye alikuwa Mfalme wakati huo, wa *Salemu*, ambayo hutafsiriwa, "Mfalme wa Amani, Shalom." Mfalme wa Yerusalemu, aliyekutana na Ibrahimu na akampa divai na mkate, ushirika, baada ya vita. Mfano bora sana hapo katika sura ya 7 ya Waebrania, tunaona. Sasa, alimpa mkate na divai baada ya vita kuisha. Kama Yeye . . .

77 Hicho ndicho kitu cha kwanza tutakachopokea baada ya kuingia katika Ufalme Mpya, tutakula tena mpya pamoja Naye katika Ufalme wa Baba, ule mkate na divai. "Sitakunywa tena uzao wa mzabibu, wala kula mkate tena hadi nitakapokula pamoja nanyi, mpya, katika Ufalme wa Baba, siku hiyo.

78 Sasa, sasa tunapotambua kuwa baada ya Mfalme Shalom kuwa katika ule. . .alipotoka kwenye huo mji, kisha kanuni ya imani ikautawala, baadaye. Na kila mara imekuwa kanuni ya imani, lakini yawakilisha lile kanisa la kale. Na tunafundishwa katika Agano Jipya, usikose kupata hili, katika Agano Jipya kuwa sisi si wa mji huu wa Yerusalemu ya duniani, lakini twatoka kwa ile Yerusalemu Mpya, iliyo juu. Kwa hivyo hii haina budi kuwa ndiyo mwezi, Yerusalemu, na sio Yerusalemu Mpya, iliyo juu. Kwa hivyo mwezi unawakilisha kanisa, kidunia.

79 Na si ajabu kuwa kabla tu ya popu kwenda zake Yerusalemu, mwezi mbinguni ulipatwa kabisa, siku chache tu kabla yeye kwenda, safari yake. Yeye pia anakuja hapa, kama mjuavyo, mwaona. Sasa hilo halijawahi kujulikana, ona. Lakini hilo laonyesha nini? Ya kuwa, hili, yeye afanya hili apate ushirika kama vile alivyokutana siku ile baada ya kuingia Yerusalemu, yeye alikutana na wakuu wa kanisa la Orthodox ya Kiyunani. Na hilo laonyesha nini? Ushirika, wao wanataka Waprotestanti na Ukatoliki waungane pamoja, ambalo wanafanya na watafaulu kabisa. Na Mungu alituonyesha haya kwa mfano, katika mwezi, kwa kupatwa wote. Kwa rehema na neema zake . . .

80 Je kuna ye yote kati yenu aliyeona gazeti ambalo walipiga picha za mwezi? Ninalo hapa. Ikiwa sio mfano kamili, ukiachilia wakati wa saba ambao u bado, vile hasa nilivyozichora kwa Roho Mtakatifu, zile Nyakati za Kanisa. Kunazo sita, ule wa saba bado haujakwisha. Zile hali sita za mwezi, jinsi ulivyong'aa katika wakati wa kanisa la kwanza; ukawa giza katika wa pili,

wa tatu, wa nne, wa tano, na wa sita; jinsi tu Roho Mtakatifu alivyoniwezesha kuzichora ubaoni, ndiposa akazitambulisha Mwenyewe ukutani mwa Masikani, miaka miwili iliyopita. Ule mwezi ulionyesha mng'ao wake, na sayansi tena ikapiga picha ya Nyakati za Kanisa, kama tu vile walivyopiga picha ya Nuru hiyo huko na kuiweka kwenye gazeti liitwalo Life, kuhusu kule kufunguliwa kwa zile Mihuri, kufunuliwa katika wakati wa yule malaika wa saba. Katika siku za huduma yake, yule mjumbe wa saba, zile siri za Mungu, siri zote ambazo zimekuwa katika nyakati zote, zingefunuliwa, zidhirishwe, inapaswa kuwa wakati huo. Naye alilitenda! Maneno Yake hayakosi kutimia. Je, si ajabu hiyo? Mungu akichora mbinguni mambo yale yale wanayoshikilia, Mungu yule yule aliniwezesha kuchora ubaoni, ndiposa akazichora Yeye Mwenyewe. Hiyo ni mara tatu Yeye amelitambulisha kikamilifu, na kabla tu papa hajaingia Yerusalemu.

81 Naam, hiyo ilikuwa kanisa, mwezi ni kanisa, huwakilisha kanisa. Na mbele ya kanisa, kivuli cha dunia hupitia mwezini. Na kivuli cha kilimwengu, kile kivuli cha kilimwengu, kanisa la kilimwengu, limetandaa kote kutia kivuli Nuru yote ya Biblia. Ulimwengu umeingia katika ile Nuru iliyoonyeshwa. Je, Mwafahamu? Ulimwengu ulipitia katika nuru ya mwezi, na kulifacha jua. Na kule kuonyesha nuru kwa mwezi kunakohitajika kutoa nuru duniani, kulitiwa giza. Naye aliingia na kuchora picha jinsi alivyofanya hasa, kwa upako, kabla haijatendeka.

82 Sasa hiyo, naamini, Dada Simpson, ilikuwa gazeti la Tucson. Sijui kama Dada Simpson alijua . . . Yeye hakulielewa wakati huo. Yeye alisema, "Nilikukatia picha, na muhtasari wa maneno, toka gazetini," akanipatia.

83 Nami nikaidhania ni jambo geni! Nikaingia humo na kuichukua na kuitazama, nikisema, "Ndicho hiki, vivyo hivyo hasa, mwaona, kile tu nimekuwa nikitazamia." Na kilikuwa pale gazetini.

84 Dada Simpson aweza kuwaambia zimo katika gazeti gani, ukitaka kupata nakala yake. [Dada Simpson asema, "La Desemba 28—Mh.] Na—na wasemaje? ["Ni nakala ya jioni ya Desemba 28"] Nakala ya jioni ya Desemba 28.

85 Mwaona, kabla yeye hajakwenda Yerusalemu kutia giza Nuru yake; au njia iliyo nayo ya kufikiwa. Saa, mahali, haki lilizo nazo za kuangaza, sasa inazikatisha zote pamoja, kwa wakati wa mwisho, ule wakati wa saba wa kanisa ambapo laingia gizani. Ni jambo kuu jinsi gani Bwana analotwambia. Katika kila kitu, haijawahi kukosa kutimia ila kile Mungu mbinguni amekitangaza na kukisema, kikatazamiwa, na hapa amekitambulisha na ku—kukithibitisha, kuwa ni Kweli kabisa.

86 Giza, wakati huu wa Kanisa la Laodikia. Sasa wakati Yesu, ambaye ni Neno, katika Wakati wa Laodikia alikuwa nje ya kanisa, akibisha mlango, akijaribu kuingia. Giza, giza kuu juu ya watu hawa. Je, Biblia ilikuwa sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina—Mh."]

87 Ukamilifu wa Maandiko, utukufu wa Jina Lake kuu. Ziara ya papa ilikuwa ishara ya makanisa kutiwa giza dhihirisho Lake. . . Ile Nuru iliyodhihirishwa ya duniani ilikuwa ni Biblia. Yesu alisema Yeye alikuwa Nuru ya ulimwengu. Biblia ilisema kuwa Yeye yu Neno. Na Maandiko yaliyodhihirishwa au yaliyothibitishwa, ni Nuru. Naam, hutaruhusiwa kufanya haya hii itakaposhika hatamu. Nasi twaona kwamba imeonyeshwa awali kwa mfano, imenenwa kwa upako wa Mungu kabla haijatendeka; imeonyeshwa awali na mwezi, na kuonyesha ikitendeka, na ndiyo hii hapa ikitendeka.

88 Wakati huo umetufika, giza, giza kuu. Giza kuu juu ya watu sasa, hivyo ndivyo ilivyo. Haya yote yamanisha nini? Tunasimama wapi? Tuko katika saa ipi? Tuko karibu vipi na kule Kuja? Vema, ninyi mwasema, "Wakati wote watakapopata ufufuo".

89 "Msiogope enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme." Vema.

90 Inamaanisha nini? Mungu ameanza kutenganisha Nuru na giza, mwaona, akilisukumia nyuma, kama alivyofanya mwanzoni, kuonyesha kupambazuka kwa siku mpya. Zile Nyakati za Kanisa zaendelea kwisha. Samahani. Nyakati za Kanisa zaendelea kwisha. Mungu analisukumia giza hadi mahali fulani, yabidi iwe hivyo, kutowesha taratibu za madhehebu, kutowesha ulimwengu. Ulimwengu unakifunika kitu hicho chote, na malimwengu yanatawala mambo yote. Basi si Mungu ni wa kweli? Kwa maana mambo ya kilimwengu, kuvalia kilimwengu, na kutenda kilimwengu, na kuishi kilimwengu, ni ulimwengu!

91 Ninyi si wa ulimwengu, watoto wadogo. Ninyi mu wa Mbinguni. Hapa si Nyumbani kwenu.

92 Mbona nitazame, kwetu sisi tulio wazee, nijaribu kutazama nyuma na kuwa kijana tena? Hatuwezi kufanya hilo. Lakini tunatazama mbele, si kutazama nyuma. Tunatazama hapa, yale yamekwisha kuwepo, nasi twataka kujua itakavyokuwa. Twaitazamia saa hiyo, tukijitahidi tuifikie.

93 Watu wengi wazuri na waaminifu siku hizi wameshanaswa katika hizi kanuni za imani, haya makanisa na madhehebu, "yenye mfano wa utauwa bali yakikana nguvu zake," kama 2 Timotheo, sura ya 3, isemavyo.

94 Giza kuu, kupofushwa kwa Israeli, kulikuwa kuangaziwa kwa Mataifa. Sasa kupofushwa kwa Mataifa ni kuangaziwa kwa Israeli. Ni kama tu Mchana na usiku; upande mmoja una giza, na

upande mwingine una nuru; ndiposa nuru hupita hadi upande ule mwingine. Kwa hivyo ule—ule mwezi ukipita ulivyofanya, na kuonyesha kwa giza la ulimwengu kukaficha nuru yake, ni dhihirisho kwetu kuwa wakati wa kanisa la Mataifa umekwisha. Kanisa linajitayarisha, limekuwa likijitayarisha kwa muda, ni wakati wa Kunyakuliwa. Maana giza linafunika Mataifa, na mapambazuko punde yatawazukia Wayahudi. Jua limezunguka toka Mashariki hadi Magharibi, nasi tuko katika Pwani ya Magharibi. Nuru yaweza tu kufanya jambo moja, kurudi Mashariki tena, upande mwengine. Mwaelewa, sivyo? [Kusanyiko lasema, "Amina."—Mh.] Nuru yaweza tu kurudi tena Mashariki ambapo ilianzia, Israeli. Mungu aliwapofusha kwa muda, lakini—lile—lile giza sasa linasukumiwa ulimwengu wa Mataifa na limefunika kila kitu. Mataifa wataukanyaga Yerusalemu hata majira ya Mataifa yatakapotimia. Yesu alisema hivyo. Na sasa yametimia, giza kuu juu ya watu! Mungu akiionyesha angani, kama Yeye alivyoionyesha duniani kabla haijatendeka. Tuko ndani yake.

95 Watu wazuri wamenaswa katika jambo hili, watu wazuri, watu waaminifu. Kama Mariamu na Yusufu, wao walikuwa waaminifu, mnaona, wakidhani Yeye yu pamoja nao, bali sivyo. Mariamu na Yusufu, ninyi mwajua, walipokuwa huko karamuni, Yesu, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, wao walidhani, wakibahatisha tu, kuwa alikuwa pamoja nao, bali Yeye hakuwa pamoja nao. Watu wazuri siku hizi hudhania vivyo hivyo, wao, watu hawa wanaojiunganisha katika hili Baraza la Makanisa, hawa watu katika madhehebu haya, wao—wao hudhani wanatenda jambo nzuri. Wanabahatisha Yeye yu pamoja nao, bali sivyo. Mnaona, watu wengi wanafikiri ya kwamba Yeye alikuwa pamoja nao waliposalimiana kwa mikono na mhubiri na kuandika majina yao kitabuni, lakini sivyo. Watu wengi walidhani, waliponyunyiziwa maji, wakapewa kipa imara, wakabatizwa katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," wakidhani Yeye alikuwa pamoja nao. Wao ni watu wazuri. Mariamu na Yusufu walikuwa watu wazuri. Lakini jambo muhimu ni kwamba, Yeye hakuwepo! Usibahatishe cho chote.

96 Nuru ni nini? Lile Neno lililothibitishwa, lililonenwa la Mungu. Nje ya hilo, hamna nuru. Mnaona? Huwezi kuangaza ulimwengu kwa mienge. Yahitaji Neno la Mungu lililodhihirishwa, yule Mwana.

97 Wao walikuwa watu wazuri. Tazama usahihi wa Neno Lake, jinsi lilivyo kamili. Je, uliona yale Mariamu alisema? Sasa kwenu ninyi watu Wakatoliki wapendwa, sina chuki nanyi. Sina chuki nanyi. Ni dhehebu mlilo ndani yake. Na ninyi Waprotestanti, vivyo hivyo. Ni hayo madhehebu!

98 "Mariamu, mama wa Mungu"? Chunguza, Mvulana wa umri wa miaka kumi na miwili, mwanawe, ilimbidi amsahihishe.

Hakuna wakati hata mmoja katika Biblia ambapo Yesu aliwahi kumwita Mariamu "mama" Yake. Yeye hakuwa mama yake. Angewezaje kuwa mama wa Mungu? Yeye alikuwa tu tumbo la uzazi alilotumia kuja duniani, adhihirishwe duniani, kwa uzazi. Hakuna chochote kwake, hakuna hata Andiko moja lililowahi kusema "mama."

99 Chunguza jinsi Mariamu alivyokosea, lakini Neno Lake ni kamilifu sana. Yeye alimwambia wakati... Alipompata hekaluni, akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, akijadiliana na wale wanatheologia. Yeye aliwastaajabisha, akiwa Mvulana wa miaka kumi na miwili; hata hajakwenda shuleni, au ikiwa alienda, hatuna habari hiyo. Lakini Mvulana wa miaka kumi na miwili akiwashangaza wa—wale watu wenye hekima hekaluni, kwa hekima Yake. Yeye alisema, "Baba yako na mimi tulikutafuta kwa huzuni." "Baba yako!" Mama mwenyewe, alivyodhaniwa, kasema, "Baba yako Yusufu nami tulikutafuta Wewe kwa huzuni."

100 Na Yeye alimwambiaje? "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwa katika kazi za Baba Yangu?" Ikiwa Yeye angekuwa akishughulikia kazi ya Yusufu, Yeye a—angekuwa akijenga nyumba, au katika duka la seremala. Lakini Yeye hakuwa mwana wa Yusufu. "Mimi niko katika kazi za Baba yangu," nikisahihisha haya madhehebu na kanuni za imani na mambo ninayoyasikia. Mwaona? "Niko katika kazi za Baba Yangu." Yeye hakukubali kuwa Yusufu alikuwa Baba Yake. Lakini Mariamu alifanya hivyo, Naye aligeuka akamnyosha.

Yeye alisema, "Baba yako na mimi tulikutafuta."

101 Yeye alisema, "Niko katika kazi za baba yangu," akionyesha kuwa Yusufu hakuwa Baba Yake. Maneno Yake ni makamilifu, mwaona.

102 Lakini Mariamu na wengineo, wakibahatisha tu hilo. Vema, mwaona jinsi ilivyokuwa, yeye alishawishiwa. Yeye—yeye alipata... Yeye alitaka kuonyesha mbele ya makuhani na wengineo ku—kuwa yeye hakuwa mwanamke wa aina hiyo. Naye, katika kufanya hivyo, aliuvunja kabisa msingi wa ushuhuda wake, baada ya kushuhudia kuwa Malaika alikuwa amemjia na kusema, "Nawe utapata mimba na kumzaa Mwana, pasipo kumjua mwanamume, Mwana aliyezaliwa kibikira." Na hapa mbele ya Baraza kuu la Kiyahudi, yeye asema, "Yusufu, Baba Yako hapa, pamoja nami, tulikutafuta."

103 Na huyo Mvulana wa miaka kumi na miwili alisema, "Mimi niko katika kazi za Baba Yangu." Yeye alimkemea Mariamu, "Huyo si Baba Yangu!"

104 Mnaona kanisa siku hizi limechukuliwa sana na mabaraza na mambo ya ulimwengu, sasa limetiwa giza. Mungu analikemea!

105 Yesu hakumwita kamwe "Mama." Siku moja Mariamu alikuja kumtembelea Yeye mikutanoni Mwake, katika mkutano wa nyumbani kama huu. Mtu fulani akaja, akasema, "Pale nje milangoni, mama Yako na ndugu Zako wanakungoja."

106 Yeye alisema, "Ni nani mama Yangu, ndugu Zangu? Ni akina nani? "Akawatazama Wanafunzi Wake, na kusema, "Wale watendao mapenzi ya Baba Yangu, ndio mama Zangu, ndugu Zangu, dada Zangu, na kadhalika. Ndio hao."

107 Na msalabani, alipokuwa akifa, alimwambia Yohana, yule mwanafunzi kijana, Yeye alisema, "Tazama, mama yako." "Bibi, tazama mwanao." "Mwana, tazama mamako." Waona, hakudai hayo, Yeye mwenyewe." Hakuwa mwanawe. Alikuwa Mwana wa Mungu. Huyo mwanamke alikuwa tu tumbo la uzazi.

108 Hii ni nyumba asubuhi hii, lakini si Kanisa. Kanisa limo ndani yenu, Kristo. Roho ya wenye kufa, wanaoketi hapa, hukusanyika pamoja katika ulimwengu wa roho. Ni Kristo, si nyumba. Nyumba ni nzuri, inatumikia kusudi lake, lakini inatumika tu kama mahali pa kukutanikia. Mariamu alikuwa tu tumbo la uzazi ambalo Yeye alitumia kuja duniani, ajitambulishe Mwenyewe kati ya watu. Si "Mama ya Mungu" kama tu vile nyumba hii isivyo Kanisa la Mungu. Inatumiwa tu kwa hayo.

109 Naam, marafiki wengi wadhani sasa, watu, watu wazuri kama Mariamu na Yusufu, hudhani kuwa—kuwa Yeye yu pamoja nao katika kutenda hili. Lakini kama wao walivyokuwa wakati huo, ndivyo walivyo sasa, wamekosea. Wao walidhani walikuwa pamoja Naye, lakini hawakuwa Naye. Lakini wao walipobatizwa, labda watu walidhani, loo, ni—nilimpokea nilipomkubali Yeye na nikabatizwa. Hilo silo. Hadi Neno lililonenwa lijidhihirishe lenyewe!

110 Lakini, Wateule, na ile Nuru sasa je? Nimekuwa nikinena mengi zaidi kuhusu giza, nami nimetumia nusu ya wakati wangu, ni saa tano na nusu. Sasa hebu na tugeuke upande mwingine; giza kuu juu ya makabila ya watu, sasa na ile Nuru, je? Yeye alisema giza kuu lingekuwa juu ya watu, lakini kungekuwa na Nuru, "Ondoka, uangaze, kwa kuwa Nuru yako imekuja." Yawezekanaje kuwe giza na Nuru pamoja, havina budi kutenganishwa. Na kitu pekee kinachotenganisha, lile Neno lililodhihirishwa, hutenganisha, hulisukumia upande mwingine wa. . .Hapa kuna lile giza duniani, lakini wakati lile Neno lililodhirishwa la Mungu, lile jua, ambalo lilinenwa liwepo kwa Neno, lijionyeshapo lenyewe, giza hukimbia upande mwingine. Na hiyo ndiyo inayotendeka sasa, giza likijitenga lenyewe kutoka kwa Nuru. Sasa kwa Kanisa lililoteuliwa katika wakati huu wa giza. . .Ambayo, tungeeleza hayo kwa masaa mengi, lakini nadhani nimesema ya kutosha hadi mwaelewa kile—kile

yale Maandiko yamaanisha, niliposema "giza kuu litafunika kabila za watu."

111 Sasa naliambia Kanisa, "Shalom: Amani ya Mungu." Amani! Kila Mwebrania wa kweli, amkutapo mwingine, "Shalom." Kwa maneno mengine, "Salamu za asubuhi! Mungu awe nanyi! Amani ya Mungu iende pamoja nanyi: "Ni Salamu za asubuhi! U hali gani?" Ni mapambazuko, Kanisa. Ni giza kuu limefunika kabila za watu. Lakini ni "Asubuhi njema" kwa Kanisa, Kristo anaonekana kati yetu. "Shalom. Amani." Haleluya. "Shalom."

112 Tuonapo giza likiingia, giza kabla tu ya kupambazuka, twajua kuwa nyota ya asubuhi inaning'inia kule, kutangulia jua linalokuja. Hapo ndipo nyota ya asubuhi inapong'aa. Ni—ni—ni kule katikati. Kila mara huwa giza sana dakika chache tu kabla ya mapambazuko, giza huja, mwezi hukoma kung'aa. Ni kweusi sana kabla ya mapambazuko, kwa sababu nuru inasukuma giza. Lakini ile nyota ya asubuhi huja na kusema, "Salamu za asubuhi. Shalom."

113 Huyo ni Yeye kati yetu, Neno Lake likitambulishwa. Shalom. Ile siku kuu inakaribia kupambazuka, asubuhi ya milele itakapopambazuka, inayong'aa sana, wateule Wake watakusanyika nyumbani mwao ng'ambo ya anga. Majina yaitwapo huko juu, nitakuwepo. Majina yetu yamo Kitabuni Mwake, tutakuwepo. "Shalom. Salamu za asubuhi. Amani iwe kwenu."

114 Giza linajitenga na Nuru. Mungu ndiye anaisababisha, Nuru inatenda hayo. Mwaona, Nuru inajisukumiza Yenyewe sana hata giza linalazimika kukusanyika pamoja. Wao walikuwa na nafasi ya kuikubali nao hawangeikubali, kwa hivyo limejikusanya lenyewe. Na wao wanafanya hivyo kwa kuunganisha makanisa pamoja, na Baraza la Makanisa, na kuungana na giza la upagani. Ingawa wao hawakubaliani kabisa wao kwa wao, iliwabidi waje pamoja ili kuuwezesha usiku kufunika makabila yote.

115 Isaya 60:1 yasema, "Ondoka, uangaze, kwa kuwa Nuru yako imekuja kwako."

116 Ondoka, uangaze, kwa kuwa ile Nuru imekuja. Neno, Nuru, limethibitishwa tena. Nuru imethibitishwa tena, Neno la Mungu, ili uweze kuona Mungu amedhihirishwa katika ahadi Yake ya Nuru ya wakati huu, au lile Neno lililotolewa kwa wakati huu, mwaona, ahadi hizi zilizofanywa kwa ajili ya siku hii, ahadi zilizonenwa na manabii, na Yesu Mwenyewe. Katika siku hizi! "Mungu ambaye alisema zamani. . ." Waebrania 1, "Mungu, alisema zamani na baba zao katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, bali katika siku hii ya Mwisho kwa Mwana Wake, Yesu Kristo." Mwaona?

117 Ile Nuru kuu iliyoning'inia jangwani ambayo ilikuwa, Musa alipoiacha Misri, akihesabu ya kuwa kushutumiwa Kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri.

118 Ndiyo ile ile iliyomkuta Sauli njiani akienda Dameski. Nuru kuu ilining'inia mbele Yake, Nuru ile ile, Nguzo ya Moto ile ile. Sauli, akiwa ni Mwebrania, hangeweza kuabudu roho ye yote wala cho chote, wala kuiita "Bwana", katika ile hali aliyokuwemo. Yeye alisema, "U nani Wewe, Bwana?"

119 Yeye akasema, "Mimi ni Yesu," (Yesu alisema, "Natoka kwa Mungu, nami narudi kwa Mungu").

120 Nuru ile ile imekuja. Kufanya nini? Kudhihirisha, ku—kuwafanya watu wajue zile ahadi ambazo Yeye ameziahidi kwa siku hii, zilidhihirisha Nuru ya siku hii. Lile giza limetiwa giza zaidi.

121 Yeye alipokuja, alikuwa ndiye Nuru ya wakati huo. Ilimpasa Masihi aje. Naye alikuja tu kama vile Mungu alivyosema atakuja, angekuja. Naye alipofanya hivyo, Yeye alikuwa nani? Nuru ya wakati huo. Nayo ikaligandamiza giza sana dhidi Yake! Sivyo? Ilimbidi Yeye atoe Uhai Wake ili ile Nuru iendelee, ipate kung'aa. Yeye alikuwa Nuru ya wakati huo. Lakini kwa nini, mbona Yeye alikuwa Nuru ya wakati huo? Alikuwa Neno lililothibitishwa ambalo lilikuwa limenenwa, likidhihirishwa. Si zaidi ya . . .

122 Mungu alinena juu ya huu ulimwengu mweusi, wenye utusitusi, wenye giza, wenye unyevu, uliokuwepo hapo bila nuru, Yeye alisema, "iwe nuru." Na hapakuwepo nuru hadi Neno hilo lilipodhihirishwa, ndipo ikawa nuru.

123 Yeye alisema, "Kutakuja Mwokozi, Masihi." Bado haikudhihirishwa hata alipokuja na kudhihirisha ahadi hiyo. Na Yeye alipothibitisha hiyo ahadi alisema, "Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake. Hayo ndiyo yanayonishuhudia."

124 Wao walisema, "Hatujui ambapo Wewe watoka, sisi tu wanafunzi wa Musa."

125 Yeye alisema, "Kama mngalikuwa wanafunzi wa Musa mngenijua Mimi maana Musa aliandika habari zangu." Mwaona? Yeye alikuwa ndiye lile dhihirisho. Yeye alikuwa thibitisho la Neno la Mungu lililonenwa na Musa.

126 Na siku hizi tunazoishi, Mungu amekuja jukwaani kuthibitisha na kuhakikisha ahadi Zake. Kwa hivyo, ni Nuru ya wakati huu, kwa hivyo twaweza kuondoka na kuangaza. Nuru tayari inaangaza juu yetu tena siku hizi, lile Neno tayari linadhihirishwa. Ni Nuru.

127 Kama tu hiyo nuru inayong'aa hapo nje, nuru ya jua, asubuhi hii. Hilo ni Neno la Mungu lililonenwa, hakuna kingine chochote kiwezacho kutoa nuru hivyo. Hakuna chochote kiwezacho kuifanya. Na nuru yo yote ya kujitengenezea hung'aa kitambo kidogo, na globu na cho chote kile. Lakini hiyo haishindwi, maana ni Neno la Mungu lililonenwa likidhihirishwa.

128 Kanuni chache tu za imani za kidhehebu zitalipua globu, kuunguza globu, na kuchoma fyuzi, na cho chote kile. Lakini Neno la Mungu halitashindwa kamwe! Litakuwa lenyewe, kila mara, lile Neno.

129 Ninasikitika nitapitisha wakati kidogo hapa. Au, au ni vema kuendelea na kumaliza ujumbe huu, sivyo? [Kusanyiko lasema, "Amina"—Mh.] Vema.

130 Ondoka, uangaze, maana Nuru imekujia. Lile Neno, Nuru, yathibitishwa.

131 Njia pekee, kama Mungu alivyokuwa, Yesu Kristo alikuwa ufunuo wa Neno lililonenwa la Mungu, ile Nuru ya wakati ule.

132 Yohana Mbatizaji alikuwa Nuru ya wakati huo. Yeye alikuwa Nuru kabla Yesu hajawa Nuru. Nabii Isaya alisema, "Sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, na yanyosheni mapito Yake." Hilo lilikuwa Neno lililonenwa la Mungu, lilikuwa limekaa hapo, lilikuwa bado kuhuishwa. Malaki, yule nabii wa mwisho, miaka mia nne kabla haijatendeka, yeye alisema, "Tazama, namtuma Mjumbe Wangu mbele Yangu, amtayarishie Bwana njia." Hapa yuaja mtu toka jangwani, hana dhehebu, hana kanuni za imani, hana kitambulisho. Lakini Nuru yake ilimtambulisha. Neno lilimtambulisha.

Wao walisema, "Je, wewe ni Masihi?"

133 Yeye akasema "Mimi siye! Lakini mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, "Itengenezeni njia ya Bwana!"

134 Yesu alisema, "Mlitembea katika Nuru yake." Yeye alikuwa Taa iwakayo na kung'aa kwa muda. Kwani? Njia ilipotengenezeka, ndipo Taa yake ilizimika.

135 Hamwezi kutembea katika nuru *hiyo*, ninyi Wabatisti. Hii ndiyo Nuru ya wakati huu! Nuru imekuja. Ondoka uangaze. Lile Neno, Nuru. Neno la Mungu lililodhihirishwa (likitambulishwa) ni Nuru.

136 Vipi sasa kwa mwaka mpya tunaoukabili? Tungekuwa na mengi ya kusema kuhusu haya hapa katikati, toka gizani hadi Nuruni, kule kujulishwa kwa Nuru kukija katikati, lakini sasa twataka kuingia moja kwa moja kwa mwaka mpya. Vema.

137 Mwaka mpya, mwaka mpya, tusemeje? Unaleta tumaini mpya. Tumekaribia zaidi kwa mwaka mmoja. Tumekuwa siku moja karibu kuliko tulivyokuwa jana. Tuko saa moja karibu zaidi kuliko tulivyoanza, dakika kumi na tano—saa tano kasorobo, ni saa sita kasorobo sasa. Tuko saa moja karibu: Hatutazami nyuma, tunatazama mbele. Mwaona? Loo! Naam, bwana. Mwaka mpya haumaanishi kufungua ukurasa mpya. Ha—ha. La.

138 Kama mtu fulani asubuhi moja; nilisikia. Mtu mmoja aliamka mapema na kutoka nje na kuchukua gazeti, akarudi, na kuketi chini, akaweka miguu yake juu ya kiti kikubwa,

akavaa miwani yake akaanza kusoma gazeti. Mke wake, huku akitayarisha kiamsha kinywa, akauliza, “Yohana, kuna jambo lo lote jipya?”

139 Kasema, “La, Mambo yale yale ya kale, watu wapya tu.” Naam. Ndivyo. Mauaji, unajisi, na mengineyo yote, mtu mwingine ameyafanya hayo, mwaona. Kweli.

140 Si kufungua ukarasa mpya. Ni kurudi kwa Neno, oneni kile Neno limeahidia siku hizi, oneni kile ile Nuru ya siku hizi inapaswa kuwa. Kile kitupasacho kutenda mwaka huu si kurudi kwa kanuni za imani na mengineyo, kurudi kwa madhehebu yetu ya kale, si kurudi kwa madhehebu hayo mazee; lakini kurudi kwa Neno, kuona ni aina gani ya Nuru inayopaswa kung’aa leo. Ee, kanisa, rudini kwa Neno, rudini kwa neno, finyeni swichi halisi, acheni kuchezea taa za umeme, mwaona, za kujitengenezea, zilizotengenezwa na wanadamu. Geukieni Neno Lake na mwone ahadi ya leo. Ndiposa angalieni ahadi ni nini na kutazamia kutambulishwa kwake. Inapothibitishwa, ndipo unajua ikiwa u Nuruni au la. Angalieni ahadi ni nini.

141 Kufungua kurasa mpya au kubadili kalenda hakugeuzi wakati. Watu wengi husema, “Vema, mwaka wa kale umepita, tupilia mbali hiyo kalenda zee ya Desemba sasa na uweke ile nyingine, mwaka mpya.” Hayo hayo ndiyo mwaka mpya humaanisha kwao.

142 Kwangu mimi, nataka kuona kile kimeahidiwa kwa siku hii. Nataka kujua Nuru ya wakati huu ni nini, ili nijue jinsi ya kuenenda kwake. Nataka nijue ninakoishi, ni wakati gani niliomo, niko umbali gani njiani.

143 Kama Paulo alivyosema, inastahili kunukuuliwa tena, “Nikiyasahau yaliyo nyuma, sasa nakaza mwendo niifikie mede ya thawabu, mwito mkuu,” hata kutambulishwa kukamilifu, ambapo wakati wote utaishia Milele Yesu ajapo.

144 Fanya kama Daudi alivyofanya, weka siku zako za usoni mikononi Mwake. Usitazame kingine cho chote, lakini weka . . . Daudi alisema hapa, yeye alisema—alisema, “Wakati wangu u mikononi Mwake.” Watambua hapa katika Zaburi tuliposoma, katika 62, “Wakati wangu u mikononi Mwake. Yeye ni mwamba wangu.” Yeye yu nini? “Yeye amefunuliwa kwangu. Yeye ndiye Kweli ilivyofunuliwa. Wakati wangu u mikononi Mwake.” Amina. Loo, mie! Naam.

145 Wakati wangu ni Wake. Mimi ni Wake. Mimi niko mikononi Mwake kwa sababu Yeye aushikilia wakati. Sijui ya usoni, lakini namjua Yeye aliye na ya usoni. Kwa hivyo, Yeye aliye na ya usoni hunishikilia. Kwa hivyo mbona niwaze kuhusu kuanzisha *hiki, kile, kinginecho* kwa huu mwaka mpya? Ninajiweka tu mwenyewe mikononi Mwake, na kuenenda kama Daudi alivyoenenda, “Wakati wangu u mikononi Mwake,” alijua kuwa Mungu alishikilia yajayo. Daudi hakujua ya usoni yangekuwaje,

lakini yeye alijua Mungu alishikilia mambo ya usoni. Sijui ya usoni yalivyo, hakuna yeyote kati yetu ajuaye. Lakini twajua Yeye ayashikilia ya usoni.

146 Subira. Subira. Wengine wetu huwa, wengine wetu huwa na haraka sana. Nafikiri watu wengi wazuri wamefanya hivyo. Unakuwa na haraka ku—kubwa. Unataka, waona, unataka kutende hayo mwenyewe.

147 Na ndugu wahudumu, mwajua ninaponena, ninyi mnaosikiza kanda hii. Nazungumza nanyi, si kwa makutano hawa wachache tu, lakini watu wote ulimwenguni.

148 Watu wengi huondoka, bila subira; lakini wakiamini kuwa wakati u karibu, unajaribu kujifanyia jambo fulani ndani yako. Mngojee Bwana. Subira ni nguvu. Ikiwa waweza kuwa na subira, ni nguvu." Ni nguru ikiwa wewe... "Wao wamgojeao Bwana waatapata nguru mpya." Sio wao wanaojaribu kwenda mbele ya Bwana, wao, wanaojaribu kumwambia Bwana, "Bwana, najua unanitaka nitende hili, Mungu atukuzwe mimi..." Usifanye hivyo. Mngojee Bwana. Biblia ilisema, "Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya."

149 Mungu alichukua maelfu ya miaka kutimiza ahadi yake ya Mwokozi ajaye. Lakini, kumbuka, Yeye alijua wakati wote, itakapotimia. Kulikuwako watu wengi waliojitokeza na kujaribu kuwa masihi. Makanisa mengi yalijaribu kuzaa masihi. Lakini Mungu alikuwa na wakati uliotengwa kwa Masihi Wake. Yeye hakuwa na haraka yo yote. Mwaona?

150 Na, katika wakati wa hili, Yeye alionyesha mifano mingi ya Masihi. Alionyesha wakati wote tangu Adamu hadi kwa Masihi, Adamu wa kwanza na Adamu wa mwisho; mmoja wao wa duniani na yule mwingine wa Mbinguni, mmoja wa kidunia na mwingine wa Kimbinguni, Mmoja alishuka kutoka Mbinguni na mwingine alitoka duniani. Lakini aliahidi Masihi, Yeye alichukua maelfu ya miaka kulitimiza.

151 Alionyesha katika Yusufu vile Yeye alivyokuwa hasa. Yusufu alikuwa mfano Wake.

152 Daudi alikuwa mfano Wake, Daudi alipokataliwa kuwa mfalme, alikwenda juu ya mlima na kutazama nyuma na kuulilia Yerusalemu, kama mfalme aliyekataliwa, huyo alikuwa Yesu katika Daudi. Miaka mia nane baadaye, yule Mfalme aliyekataliwa alisimama juu ya Yerusalemu, akasema "Yerusalemu, Yerusalemu, mara ngapi nimetaka kuwakusanya ninyi kama kuku avikusanyavyo vifaranga wake, lakini hamngekubali."

153 Mtazame Yusufu, alizaliwa kati ya ndugu zake, wale wazee wetu; si yule wa mwisho (anayefuatwa na kitinda mimba; Benjamini alikuwa kitinda mimba). Lakini kabla tu yule wa mwisho, mwaona, kabla tu ya huyo. Alichukiwa na ndugu zake, akapendwa na baba yake. Yeye alichukiwa kwa sababu

alikuwa mtu wa kiroho. Angetafsiri ndoto, zilikuwa kweli hasa. Angeona maono, angetabiri mambo ambayo yangetendaka. Na wao walimchukia. Aliuzwa kwa vipande thelathini vya fedha.

154 Walimchukia Yesu kwa nini? Walimwita Yeye Beelzebuli kwa sababu Yeye alikuwa Neno, na Neno laweza kupambanua mawazo yaliyomo mioyoni. Walimchukia Yeye. Na wao walimuuza vipande thelathini vya fedha.

155 Yeye alitupwa shimoni, Yusufu alitupwa, wakadhani amekufa. Koti lake lililolowa damu liliachwa nyuma, kama vazi la Yesu lililolowa damu na kutwaliwa kutoka msalabani, joho alilovaa, kutambulisha kifo chake. Lakini Mungu alimfanyiaje Yesufu? Yeye alimtoa shimoni, na kumweka kwenye mkono wa kuume wa Farao. Na hakuna mtu angemwona Farao, ila amwone Yusufu. Na Yusufu alipoacha lile jumba la enzi, tarumbeta zilipigwa na tangazo lilitolewa, "Kila goti lipigwe, Yusufu anakaribia."

156 Vivyo hivyo, Yesu. Yeye alitolewa toka shimoni, ambamo ilidhaniwa amekufa, na alifufuliwa na yuaketi mkono wa kuume wa Nguvu. "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote, ila tu yule Mwana mpendwa wa Baba. Na aondokapo hapo, tarumbeta zitapigwa, na kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri." Mnaona, Yeye yu Mfalme wa ustawi. Tazama yale Misri ilitenda wakati huo, iliuokoa ulimwengu mzima, kiangazi kilipokuja. Kwa hivyo, ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu ajapo. Goti, kila goti litapigwa na kila ulimi ukiri ya kuwa Yeye yupo.

157 Yeye alionyeshwa kote kote katika mifano, lakini Mungu alijua hasa wakati Yeye angekuja. Alijua hasa Yeye atakapokuja. Haijalishi walikuwa na wangapi hapo kabla, Yeye alikuwa na Masihi Wake. Yeye aliwaonyesha katika mifano, kile kitakachokuja.

158 Ni vivyo hivyo tu alivyotuonyesha sisi zile Nyakati saba za Kanisa, kile kingekuja. Ni kama tu vile Yeye alivyotuonyesha kile kingekuja Yeye alipoielekeza Nuru hiyo huko juu, katika Ufunuo Wake, kuonyesha ulimwengu. Yeye alipotuma wale Malaika saba kufunua wale wajumbe saba waliokuwa kote nyuma huko, na kuonyesha yale yaliyoachwa, kila Malaika akija kila siku na kufunua yale yaliyoachwa na Luther, na yaliyoachwa na Wesley, na yaliyoachwa na Pentekoste, yote yamewakilishwa ndani humo. Na katika mfano halisi na kivuli cha Shalom mkuu, Yehova, Jvhu. Mwaona? Hakika. Akaitandaza angani, na hapo kuna macho ya mashine yakichukua picha Yake. Mwaona? Bwana ashukuriwe!

159 Shalom! Amani! Msichoke, Yesu yuko hapa. Nuru Yake kuu imetujia, nasi twashukuru kwa ajili yake, naam, Neno Lake, ile siri kuu. Ndiye huyu hapa leo akijidhihirisha mwenyewe,

akitenda mambo yale yale Yeye aliyoyatenda wakati huo, vivyo hivyo tu. Akitenda jambo lile lile.

160 Sisi ni viumbe vya wakati. Yeye ni Mungu wa Milele. Tunajaribu kujitahidi, twajaribu kufanya kitu fulani tofauti, "Loo, hili lapaswa litendwe." Kumbuka, Yeye ajua yote kulihusu. Litatendeka, kwa vyovyote. Mwache alitende. Jikabidhi tu Mwenyewe Kwake.

161 Inua macho yako, ukaangaze kwa furaha ya Bwana, kujua kuwa umejaliwa, macho yako yamefunguliwa na kuona siku hii. Mtumainie Yeye kwa ya usoni. Mmemwona Yeye akithibitisha Neno Lake katika siku zilizopita. Yeye aliyethibitisha Neno Lake katika siku zilizopita na kuvifanya vitu hivi vingine vyote vitendeke kulingana na saa tunayoishi, kila kitu vivyo hivyo, kulingana na ule Ujumbe wa malaika wa saba, akayaonyesha mbinguni na duniani pia, na kuyajulisha kwa njia tatu ili kusiweko kosa, kumbuka, Yeye aliahidi angerudi tena. Haleluya! Neno hilo litathibitishwa. Neno la Mungu lililoahidiwa, pamoja na miaka elfu mbili ya kungojea, Yeye atawasili wakati ufaao! Msichoke, Yeye atakuja. Kama alivyolithibitisha Neno Lake katika kila wakati, zile Nyakati za Kanisa zote zaonyesha jambo lile lile, na kule kufunuliwa kwa Bwana na ule Ujumbe wa saba na mengineyo. Mungu alilifunua, alilidhihirisha, na kulithibitisha. Na kati yetu leo, Yeye alijionyesha Mwenyewe hapa pamoja nasi, na kuthibitisha na kuhakikisha Neno Lake. Basi atafanya hivyo!

162 Kutakuwako Utawala wa Miaka Elfu. Wazee watakuwa vijana huko milele. Magonjwa yataisha na kifo hakitakuwako tena. Watajenga nyumba, watakaa ndani yake. Watapanda bustani za mizabibu na kula matunda yake. Hawatapanda na mwingine arithi (mwanawe aichukue), mwanawe atakuwa akiishi pamoja naye. Yeye hatapanda na mwingine ale, afe na mwingine aichukue; lakini yeye ataishi humo. Amina! Mbwa-mwitu na mwana-kondoo watakula pamoja, na simba atakula majani kama ng'onbe, na mtoto atawaongoza, watakuwa—watakuwa wasiodhuru, watakuwa . . . Hakutakuwa na cho chote kiwezacho kudhuru. Tutageuzwa toka kwa kile tulicho sasa, tupate kufanana na na mwili wa Utukufu wa Mwana wa Mungu usioharibika, usiokufa. Miaka haiwezi kumgusa kamwe, uzee hauwezi kumfanya cho chote kamwe, yeye ni Mwana wa Mungu asiyeharibika. Kwa hivyo twajua kuwa—kuwa tuko wakati wa mwisho. Tuko katika njia panda. Mambo haya yote yametambulishwa kikamilifu, kwa hivyo yatatambulishwa tena.

163 Sasa, ya usoni, Yeye anayashikilia. Najuaje ni lini atakapokuja? Yeye atakuja lini? Sijui, lakini atakuja. Hiyo ni kweli. Yeye atafanya lini hiki na kile? Laana itaondoka lini duniani? Lini hizi onyesho zilizobarikiwa za upendo wa Mungu, za miti ikisimama hapa na kung'aa na maua na kadhalika, ni lini yasiyoharibika yatakua? Sijui, lakini itatendeka. Lini

kuonyeshwa kwa hamu ya wanadamu kuishi, na mahospitali na madaktari na upasuaji, na kulia na huzuni, vitakoma lini, kufikia utawala wa utukufu pamoja na Yesu kwa miaka elfu ya Shalom? Itakuwa lini? Sijui. Yeye alisema itakuwapo. Sijui jinsi Yeye atakavyoitimiza, lakini Neno Lake lililonenwa litathibitishwa wakati lile Jua la haki litakapozuka lenye kuponya katika mbawa Zake. Na uponyaji huo hautakuwa wa mwili, kama mnavyodhania, kama tuseme mtu fulani ana ugonjwa na utaondolewa kwake. Hilo ndilo Yeye analofanya sasa, katika mfano. Lakini kiumbe chote kitageuzwa: Huu uharibikao utavaa usioharibika. Uzee huu utaruka uingie ujanani. Amina. Vema, itakuwaje? Sijui, lakini itakuwepo.

164 Mimi mwenyewe, ninazeeka. Mwaka huu, Mungu akinijalia niishi hadi Aprili 6, nitakuwa na umri wa miaka hamsini na mitano, mzee. Lakini sitarajii. . . sitaki niwe mvulana tena. Nataka nikaze mwendo niifikie mede huko ng'ambo, kwa kusudi lile lililonileta. Karibu miaka thelathini na kitu sasa nimesimama nyuma ya deski hii, tangu mvulana mdogo wa umri wa miaka ishirini na kitu, karibu ishirini na mmoja, ishirini na miwili, nimejaribu kuutangaza Ujumbe huu. Na kila wakia wa nguvu zangu nimeuweka Kwake. Mabega yangu yakiinama na nywele zangu zina mvi na zang'oka, sitazami nyuma kwa ujana, uzee utarudi tena. Natazama kule ng'ambo kwenye kupambazuka kwa siku ambayo Neno lililothibitishwa la Mungu lilisema "hakuna hata unywele mmoja wa kichwa chako utakaoangamia, nami nitaufufua tena siku za mwisho." Yeye atafanya hivyo vipi? Sijui. Lakini natumainia . . .

165 Huu mwaka mpya, sijui kile unashikilia, lakini najua Yeye aushikiliaye. Hayo ndiyo matumaini yangu ya mwaka mpya. Yeye akija, Amina. La, haji, nitakuwa ningali nikifanya kazi Yeye akinijalia. Nayakabidhi ya usoni Kwake. Sijui yalivyo, nayakabidhi Kwake tu. Mmemwona Yeye akithibitisha Neno Lake, kwa hivyo mwajua itatendeka. Neno Lake!

Wasema, "Ndugu Branham, unalipataje hilo?"

166 Vema, hebu nikupe wazo fulani hapa kwa dakika moja. Je, mwajua tarabu ni nini? Najua mwajua. Ni muziki, ni mchezo. Mwaona, wanauigiza.

167 Sasa, ninyi watoto wadogo, ili muelewe. Mwakumbuka shu—shuleni, naamini mna . . . Unaitwaje ule muziki mdogo wa tarabu ya Kirusi, wakati mwingine wao—wao huuigiza kwa ngoma, mwajua inaitwa, si ni . . . kuhusu yule—yule gogota mdogo, mwajua, aliyeingia msituni; na wao walikuwa na kupigapiga mbawa na kupiga ngoma na vitu vingine. Na unaskia yote unaposikiza hiyo tarabu wanapoicheza. Nasahau jina lake. "Petro na Mbwa Mwitu." Naam. "Petro na Mbwa Mwitu." Sasa hiyo ni-hiyo ni tarabu ya Kirusi. Mwaona, wao hawana—hawana vitu vidogo-vidogo vikipuruka hapa na pale vikiucheza, lakini

wao huucheza kwa ngoma. [Ndugu Branham agonga mbao fulani—Mh.], na kisha [Ndugu Branham agonga kitu kingine], na kufanya ngoma na sauti na vingenevyo. Kuucheza, kuuigiza. Kwa hivyo utaelewa kile Ndugu Branham anachojaribu kusema. Mwaona?

168 Sasa kwenu watu wazima, Maandiko ni tarabu ya Mungu. Naam. Haleluya. Mtungaji tu ndiye ajuaye maana yake hasa na Yeye huifunulia wale wanaosikiza, walio na hamu ya kujua huo mchezo wa kuigiza ni nini. Lakini itakupasa kujua hiyo tarabu kwanza, waona. Si kitu fulani unachokiona tu, ni—ni kugeuzwa, mwungano wa Neno, wa muziki. Unarusha; wakati mwingine unaendelea *hivi* kwa kitambo, mdundo fulani, wakati mwingine unabadilika wote. Ni nini? Kwenu ninyi ambao hamngeuelewa au hamjui lo lote Kuuhusu, hampendezwi Nao, ni udanganyifu tu, ni udhia. Lakini wale wanaoujua, wanautazamia, wao wanajua unakuja. Haleluya!

169 Sasa tuna nyakati hizi za tarabu za Tarabu ya Neno la Mungu, hata mchezo wote wa kuigiza umebadilika. Ninyi mnaoupenda, sikizeni badiliko hilo. Mwajua linakaribia. Mwasikia jinsi ngoma zinavyopigwa, amina, mnataka kitu fulani kitendeke. Mwajua hili ni badiliko, mwaona, linaendelea kufikia mlipuko katika muda wa dakika chache. Mwaona? Na mnalitazamia, mwaweza kutambua jinsi ngoma hizo zinavyopima wakati. Ee Mungu! Ikiwa mwaweza kusikiza ngoma za kumalizia sasa, mkiweza kusikia mwangwi wa muziki wa Neno la Kimbinguni ukiimba kumalizia, "Na itakuwa katika siku za mwisho!" Ile tarabu ya mchezo mkuu wa kuigiza wa Mungu ambao anacheza, inambadili, tarabu Yake kwenye muungano. Mtungaji na wao wanaovutiwa nayo husikiza badiliko. Hivyo ndivyo jinsi vitu hivi vilivyo kwetu, tunasikiza, tunatazama. Kila wakati Yeye anapoonekana, kitu fulani hutendeka, twaona wakati ukikaribia. Twaona nyuma huko si muda mrefu uliopita wakati zile Nyakati Saba za Kanisa zilipokuwa zikichorwa, tulikuwa tukisikiliza. Tuliziona zikiambatana na Neno zikipiga sawa na Neno. Muda si muda; kipi kilitendeka? Hapa Yeye yuaja, Mwenyewe, na kulithibitisha.

170 Tulisikia Neno likisema ya kwamba, "Isipokuwa katika siku za malaika wa saba." Katika Wakati wa Kanisa, Yeye alisema tu, "Ujumbe wa Malaika wa saba utakuwa Ujumbe wa mwisho." Ndiposa, loo, twaona hapa katika Ufunuo 10, "Katika siku za Ujumbe wa malaika wa saba, zile siri za Mungu zitatimizwa," ule Muhuri wa Saba ungefunuliwa. Wakati huo umefika. Mara tu, unapotendeka, ono lilitokea, kasema, "Kwenda Tucson, mshindo mkuu utatokea wakati huu upate kuelewa kabisa na kujua kuwa umetumwa. Karibu utaitikisa nchi." Nyote mwajua hayo. Ilinaswa kwenye kanda miezi mingi kabla haijatendeka.

Ndiposa ikatendeka! Kisha ikaonekana angani. “Shalom!” Ni nini? Ni kubadili sauti ya muziki wa tarabu.

171 Ndipo wakati mmoja Yeye alisema kuhusu ule Mvuto wa Tatu; jinsi ungetendeka kwa njia hii moja, halafu kwa kujua moyo, ndiposa lile Neno lililonenwa.

172 Yesu alisema, “Naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.” Yohana 14, “Kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.” Kama tu nilivyosema muda mfupi uliopita, Mariamu alipojaribu kumtambulisha Yeye kama mwana wa Yusufu, Yeye alimsahihisha. Maneno Yake hayawezi kushindwa! Yeye alisema hivyo, Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe.”

173 Tunaposikia tarabu ikipigwa, ikibadilishwa, ikiwa tayari kubadilishwa, ni wakati wa makutano. Tunatambua Yeye anapoanza kupiga, nasi tumeona, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, naam, na kubwa kuliko hizo mtafanya.” “Kubwa kuliko,” Yeye aliliahidi. Tulishangaa ingekuwaje.

174 Lakini mlitambua Yeye alipofanya muujiza Wake wa kwanza, Yeye alichukua maji na kuyageuza yakawa divai. Sivyo? Alichukua maji, ambayo huenda yangekuwa divai siku moja, lakini yalikuwa maji kwanza.

175 Na Yeye alipolisha elfu tano, Yeye alifanyaje? Alichukua kitu fulani ambacho kilikuwa kama yale maji, Yeye alichukua samaki ambaye wakati mmoja aliogelea na alianguliwa kutoka kwa yai, naye akamvunja, na samaki mwingine akakua kwenye uumbaji ambao ulikuwa wa asili. Yeye alichukua mkate ambao kwa wakati mmoja ulikuwa ngano, na ulikuwa mbegu na ukawa mkate, akauvunja na uumbaji ukazidishwa tu.

176 Lakini mwituni hakukuwa na cho chote huko cha kutengenezea yule kuchakulo. “Na kuwe,” kukawa, pasipo cho chote cha kuvunjia. Ni nini? Yesu Kristo yule yule! Mwaona? “Kazi kubwa kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.” Si kuchukua kitu fulani ambacho kimeumbwa, kuvunja kitu fulani toka kwacho na kuongeza uumbaji, lakini kuumba kabisa. Kuonyesha kuwa Yeye ni Yehova yule yule aliyesimama hapo na kusema, “Na iwe,” na ikawa. Neno Lake likadhihirishwa! Yeye alipofanyika mwili duniani, alichukua viumbe Vyake vya asili, akavivunja na kuvizidisha. Lakini sasa katika siku za mwisho, Yeye ashukapo kati yetu tena, Nuru ile ile iliyoshuka chini, kasema, “iwe nuru,” mwaona, Yeye anena tu kiumbe na kinakuwako. “Kazi kuu kuliko hizi mtazifanya, maana nakwenda kwa Baba Yangu,” Kumbuka, tuko kwenye nyakati hizi.

177 Na ulimwengu haufahamu, kwa sababu ni “upuzi mtupu.” Kwa sababu hayo si ya Wamethodisti, Wamethodisti

hawayafahamu. Kwa sababu ati, hayo si ya Wabatisti, Wabatisti hawayafahamu. Kwa sababu si ya Kikatoliki, Wakatoliki hawayafahamu. Kwa sababu si ya Kipentekoste, Wapentekoste hawayafahamu.

178 Lakini wale wanaomngoja Bwana, wale wanaotazamia! Hamna mtu hata mmoja katika historia ya uchunguzi wa sayari, aliyejua ile Nyota ilipita kule juu. Lakini wale mamajusi waliifuata kwa maili mia kadhaa, kwa miaka miwili, wao waliitazama na kuifuata. Mwaona ninalomaanisha? Ni kwa wale wanaoisikiza hiyo tarabu.

179 Kumbuka, Mtungaji ajua mwisho tangu mwanzo. Yeye ajua yote kuuhusu, hiyo ndiyo sababu Yeye auandika hapa. Sahihi. Basi lazima uanze pamoja Naye, lazima uanze. Ukitaka kusikia ulinganifu wa sauti, unaanza Naye kama katika muziki wa tarabu. Unasikiza, unajua usemavyo, hiyo ndiyo tarabu, ndipo unaanza kusikiza muziki. Na unajua jinsi ulivyo, kwa hivyo unajua tu kuwa, "Hapa ndipo kitu *fulani* hutendeka. Sasa huna budi ubadilike." Sasa, kwa ye yote ambaye hajui cho chote kuhusu haya. . . aliingia tu na kuketi, ni mambo ya upuzi tu, makelele ya kupayuka-payukwa. Lakini yule ajuaye jinsi ilivyo, ni mapigo ya muziki, inachezwa kulingana na mlio wa ngoma, una—unapigwa kwa tarumbeta, unapigwa kwa kinubi, unapigwa kwa fidla, unapigwa kwa sauti nene, unapigwa kwa tarumbeta, unapigwa kwa ngoma. Kitu hicho chote kina mdundo, na inafanya ule—ule mfululizo wa sauti hadi unaweza kufumba macho yako na kuishi ndani yake. Haleluya!

180 Mwanadamu aweza kufumba macho yake yaharibikayo asione ya kidunia na aishi katika Uwepo wa Yesu Kristo, unapoona Neno Lake likipigwa katika tarabu tunayoishi kwake sasa, ikibadilishwa. Lazima uanze katika hiyo Tarabu. Jambo pekee uwezalo kufanya ukiwa katika hiyo Tarabu, ni kuanza, anza kuingia katika mdundo huo. Hivyo ndivyo ufanyavyo kwa Mungu. Husimami tu kando na kuitazama. Unaingia katika mdundo Wake! Unaingiaje humo? Unazaliwa Humo, katika mdundo wa Neno, unapokuwa sehemu ya Neno hilo.

181 Ilikupasa uwe sehemu ya dansi ili utoke dansini. Yakupasa uwe sehemu ya mchezo wa mpira, kitu fulani unachopendelea, ili uingie mpirani.

182 Yakupasa uwe sehemu ya Neno, ili ujue Tarabu ya Mungu. Tarabu Yake ni wakati inapochezwa, wafahamu, unaenenda katika hatua za wakati huo. Unaitazamia, "Kazi nifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo mtazifanya," siku hizi za mwisho. Lo, jamani! Kubadilika kukuu kwa wakati. Tunaingia katika mdundo ule, mdundo wa Neno. Tafuta kusudi Lake, saa tunayoishi. Ingia katika mdundo wake, niaje. . . niaje Yeye anavyofanya. Ukiingia katika Neno, utaona

jinsi ilivyofanya mwanzoni, ndipo utajua jinsi Yeye anavyotenda wakati wote.

183 Yeye alitumaje Ujumbe Wake, mara ya kwanza? Yeye hufanya nini? Yeye hashughulikii madhehebu. Hajapata kufanya hivyo, kwa hivyo Yeye hafanyi hivyo sasa. Hapo ndipo ikiwa unasikiza mdundo wa mwenendo wa Baraza la Makanisa, wewe uko gizani. Lakini ukiwa unasikiza mdundo wa Neno!

184 Sababu gani walimwua Yesu? "Wewe, uliye Mwanadamu, wajifanya mwenyewe Mungu."

185 Mliupata Ujumbe wangu juu ya *Zile Tabaka Tatu za Waamini*. Jinsi mmoja alisimama hapo na . . . Kulikuwako na waamini wa kujifanya tu, waliufuatilia kwa muda mchache, wakifanya kwamba waliamini. Na siku moja Yesu aliwaambia, akasema, "Mtasemaje Mwana wa Adamu, atokaye Mbinguni, atakapopaa kurudi Mbinguni? Nalitoka Mbinguni, narudi Mbinguni."

186 Naam, umati uliondoka na kusema, "Neno hili ni gumu."

187 Ndipo kukaja waamini wa kujifanya tu waliokuwa wakitembea pamoja Naye, wale sabini, walipopata kitu fulani kigumu, hawakuona kuwa ilikuwa . . . hawakujua hiyo Tarabu. Hawakujua ile ahadi, kuwa huyu Mwana alikuwa Yehova, "Naye ataitwa Jina Lake, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu." Na Yeye aliposema, "Nipaapo Mbinguni ambako nilitoka."

188 "Vema," wao walisema, "Neno hili ni gumu. Ni nani awezaye kulisikia? Twajua Wewe u Mwanadamu tu. Tunakula pamoja nawe, tunalala nawe, huwa nawe mwituni, huwa kando ya maji pamoja nawe. Vema, Wewe Mwanadamu tu, unasema Mwana wa Adamu anarudi juu alikotoka? Mtasemaje? Hili ni neno gumu!" Mnaona, hawakujua huo mdundo. Hawakujua mdundo wa Tarabu ya Neno la Mungu, kuwa Yeye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, maana Yeye alikuwa lile—lile Neno Nuru lilothibitishwa ya wakati huo. Hawakulipata. Wao walisema, "Hili ni jambo gumu. Ni nani awezaye kufahamu Hili?" Na wakaondoka. Hawakuelewa huo mdundo, mwaona?

189 Kisha tunaona tena, kulikuwako na Yuda, yule mwamini wa kujifanya au asiyeamini, aliyengoja hadi alipoona kosa. Ndipo Yeye akawageukia wanafunzi, akawaambia tu wale kumi na wawili, na Yuda alikuwa mmoja wao, Yeye alisema. "Ninyi mwataka kwenda pia?"

190 Basi Petro akasema, "Tumwendee nani, Bwana? Wewe u Mtungaji." Amina, "Unajua jinsi inavyoendelea. Wewe ndiwe pekee uliye na Neno la Uzima. Tugeuke twende wapi? Hatungerudi kwa Mafarisayo, au Masadukayo, au Waherode," au cho chote kile. "Wewe ndiwe uliye Neno la Uzima. Hatuna mahali pengine pa kwenda. Tume—tumejiunga wenyewe na Tafrija hii kuu. Tuko ndani hapa, tunasikiza, na tuko katika

mdundo huo. Twaamini kuwa wewe u Mwana wa Mungu, Yahova aliyedhihirishwa. Tuna hakika ya hili! Hatujui jinsi haya majaribu makuu na taabu, na mateso na kadhalika, na kusema Kwako kuwa Wewe 'unakwenda kutolewa sadaka', na yote *haya, yale,* na *mengineyo*; 'siku ya tatu', mambo haya yote. Hatuelewi hayo. Lakini tuko ndani, tukisikiza Tarabu ya Mungu, sisi tu sehemu yake. Nasi twangoja kuona kile kitakachatendeka baadaye, nasi tunakufuatilia karibu sana." Loo Jamani! Hilo ndilo ninalotaka kutenda. Ahadi.

191 Yeye alianzaje? Kama tu vile Yeye alivyofanya mwanzoni. Mwaona? Hajapata kutuma Ujumbe Wake kwa dhehebu fulani. Hajapata kutumia kundi Lake Ujumbe, alimtuma Mtu mmoja. Katika siku za Nuhu, ilikuwa ni Nuhu. Katika siku za Musa, ilikuwa Musa.

192 Kuna wengine waliodhani wakati mmoja, hata walisema, "Vema, ungejifanya mwenyewe mtu pekee aliye mtakatifu katika kundi hili." Mungu alichukia hayo.

193 Musa alikwenda kwa Bwana, "Nimetenda hili. Nini, yanipasa nitende nini?"

194 Yeye alisema. "Jitenge nao. Nitayashughulikia yale mengine. Nalikutuma. Ni wajibu Wangu." Kisha akafunua ardhi na kummeza Kora na hao wakaidi wote. Kila mara.

195 Yohana na Yesu, hawangekuweko wakati mmoja. Yesu . . . Yohana alipoinua macho yake, yeye alisema, "Naam, mimi sina budi kupungua, bali Yeye kuzidi. Yeye ndiye Nuru iliyothibitishwa." Kwa hivyo Nuru hii haina budi kuendelea hadi thibitisho kamili lije. Naam. Hiyo ni kweli.

196 Yeye yuko vile alivyokuwa mwanzoni. Hivyo ndivyo unavyoanza, jinsi unavyoanza kujifunza jinsi Mungu alivyokuwa. Yeye alifanyaje alipokuwa hapa duniani? Aliishi maisha ya namna gani? Yeye alikubali, Yeye alikuwa mtu wa kupatana? Je, Yeye alikwenda madhehebuni? Yeye alijitambulishaje? "Mwayachunguza Maandiko! Mnadhani . . . kwamba ninyi mna Uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia." Mwaona, hilo ni jambo lile lile leo au wakati mwingine wo wote. Unapotaka Nuru, angalia kile Maandiko yasemacho juu ya wakati huu. Vema.

197 Unaanzia wapi, basi? Ikiwa kuna mwenye dhambi hapa, unaanzia msalabani unapojitambua mwenyewe mfu pamoja Naye. Umejiunga basi na—na mchezo huo mkuu wa kuigiza. Unasikiza, basi, unatazama karatasi yako unapoishikilia mkononi mwako, ile—ile Tarabu. Wewe una karatasi mkononi mwako ambayo ingekwambia mambo haya, ambapo badiliko la muziki huanza kutia fora na kuigwa, ndipo unaona mchezo huo ulivyo. Uonapo Roho wa Mungu akishuka juu ya watu na kutenda jambo fulani, unatazama nyuma na kuona ilipo. Angalia kama ndilo hilo, ikiwa hilo ndilo jambo la wakati huu.

Naam, walikuwa na karatasi mikononi mwao Yesu alipokuja, ya Tarabu. Bila shaka walikuwa nayo.

198 Ninalitamka neno hilo vema, symphony, sympathy? Natumaini hivyo. Kwa hivyo basi nimeliwazia tu hilo. Symphony? [Mtu fulani katika makutano asema, symphony—Mh.] Symphony. Sivyo? Vema.

199 Sasa, wao walikuwa na karatasi mikononi mwao, lakini wangefanyaje? Wao walikuwa wakijaribu kutazama nyuma kwenye pigo lililokuwa na yote. . .sehemu fulani iliyokuwa imechezwa. Hivyo ndivyo makanisa hufanya siku hizi. Wao wanatazama nyuma na kuona ni sehemu gani Luther alicheza; Walutheri hufanya hivyo. Hawajui badiliko la muziki. Hawajui kile Mungu anatenda leo Yeye anapofanya mambo haya, Walutheri. Wapentekoste husema, "Loo, tunayo." Mna karatasi iliyochezwa miaka hamsini iliyopita. Mwaona? Hakika. Na tuliweke tu Neno hili mikononi mwetu, na kutazama badiliko lijapo, ndipo tutajua tunachotenda.

200 Sasa, basi anza pamoja Naye msalabani. "Tubuni mkabatizwe kwa jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea muziki huo, yale Maelezo," mwaona, "Neno Lake, Roho Mtakatifu anayedhihirisha Neno." Ndipo ufuatishe mdundo wa Neno. Cho chote Muziki unachocheza kwa wakati huo, cheza pamoja nao. Waona?

201 Watu wengi waliuliza, "Kwa nini?" Wao waliuliza. Wao waliuliza, wakati mwingine wao huniuliza, "Kwa nini? Kwani mambo *haya* yatendeke? Nini, kwani, mbona hili lilitendeka kwangu? Mbona nilianza na *hili* likatendeka, nami—ni—nilikuwa na shida hapa, na *hili* laniudhi hapa, na nilipoteza hiki hapa?"

202 Wakati mwingine nimeuliza, "Mbona?" Kwa nini, nilipokuwa tu mhudumu kijana, nilipoanza, Mungu alimtwaa mke wangu, chini yangu, akamchukua mtoto wangu chini yangu, chini ya moyo wangu? Mbona Yeye alifanya hilo? Sikujua. Najua sasa. Niliuweka tu mkono wangu ndani ya Wake na kuendelea kumtumai.

203 Yeye ajua kila njia panda. Yeye ajua mdundo hauna budi. . .unapopaswa kuchezwa. Yeye ajua kile kihitajikacho kukufinyanga wewe, Yeye ajua vifaa atakavyotumia. Waona? Huko upande wa nyuma wa jangwa wakati mwingine, ambapo Mungu huwafinyanga watu wenye haki wakawa wenye hekima nyingi na manabii. Mwaona? Mwaona? Hapo ndipo watu wanapoundiwa. Watu huundwa, katika Neno. Wanapokuwa na kila namna ya kanuni za imani na mengineyo ndani yao, hebu na walijie Neno na Mungu anayatwanga kuyaondoa kwao, na kuwaunda wawe Hili, kuwaingiza katika Tarabu, ya Neno Lake. Mwaona? Ndiposa wao huona Neno likiendelea.

204 Mungu ajua wakati mdundo wake huna budi ubadilike. Yeye ajua jinsi mdundo unavyoendelea. Sijui jinsi unavyoendelea, lakini Yeye ajua. Anajua jinsi unavyoendelea, sijui. Lakini nautazama hapa, na kusema, "Vema, unakuja tu."

205 "Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humwokoa toka kwa hayo yote." Waona? Mungu ameendelea katika historia yote na mdundo wa ahadi ya Neno Lake. Katika kila wakati, katika mdundo huo huo, akitimiza Neno Lake. Hivyo ndivyo Mungu alivyoendelea kote katika historia toka huko Mwanzo mpaka Ufunuo, Yeye ameendelea kote katika historia pamoja na Neno Lake. Naam, katika mdundo wa—wa nguvu za Roho Mtakatifu akithibitisha Neno Lake kwa Wateule. Kumbuka, Yeye hajawahi kugusa kanisa la nje. Ni wateule tu.

206 Watazame hao makuhani, walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye ni mpiga ramli. Naam, Yeye—Yeye—anasoma mawazo yao."

207 Hawakujua kuwa, "Neno lina ukali kuliko upanga wenye makali, ukatao kuwili, hugawanya mawazo yaliyomo moyoni." Naye alikuwa Neno.

208 Lakini huyu kahaba akisimama kisimani siku hiyo ateke ndoo ya maji, alisema, "Naona ya kuwa Wewe u Nabii. Twajua Masihi yuaja. Hatujakuwa na manabii kwa miaka mia kadhaa, lakini twajua Masihi yuaja. Naye ajapo, hivyo ndivyo atakavyokuwa."

209 Yeye alisema, "Mimi ndiye." Hilo lilitosha. Kwani? Huo mdundo ulilingana! Yeye alikuwa akitazamia badiliko hilo, toka kwa kanisa dhehebu hadi kwa Masihi aliyethibitishwa. Ndiye huyu hapa amesimama, Yule Masihi ambaye Musa alinena habari zake, "Bwana Mungu wenu atamwondokeshea nabii aliye kama mimi." Ndiye huyo hapo. Ule mdundo ulibadilika, yule Mzao aliyethibitishwa akautambua.

210 Na wakati Neno halisi la Mungu liangukiapo juu ya yule Mzao, aliyethibitishwa, kisha wakaona thibitisho hilo la Neno, hulitambua. Wanalitazamia Neno, wanajua hayo makutano, wanajua ule wakati, wanajua badiliko, wanajua mdundo unaohitajika kuwepo kwa saa hiyo. Haleluya! Wanajua ule mdundo, wanajua ile saa, wanajua jinsi inavyohitajika iende. Mwaona, wateule tu ndio wanaojua.

211 Filipo alipouona, hangeweza kujizuia tena, Yeye alijua huyo alikuwa Masihi. Kwa hivyo yeye alikwenda kwa mwenziwe, ambaye walikuwa wamejifunza Biblia pamoja naye. "Nathanieli," yeye alimwita, "njoo, mwone Mtu. Njoo, umwone yeye tuliyemwona, tumemwona Yesu wa Nazareti. Tulimwona Yesu wa Nazareti, huyo ndiye Nabii ambaye Musa alinena habari zake kuwa angekuja. Tumempata, tumempata."

212 Yeye alisema, "Yawezekanaje? Mimi tu. . . Yeye alikuwa wapi? Mwaona, yeye hakuwa. . . Mwaona, yeye hakujua ule

mdundo vizuri. Wao walikuwa wakisoma. Lakini alipofika hapo, yeye akamwambia, akamjulisha lile Neno.

213 Naye alipofika hapo, Yesu alisema, "Tazama Mwisraeli," ule mdundo ulianza kushika, ule mchezo mkuu ulikuwa ukichezwa hapo jukwaani, au sakafuni, siku hiyo. Labda Yesu alikuwa akisimama mwambani, akiwazungumzia watu. Na Filipo alipokuja pamoja na Nathanieli, Yeye alimtazama, na kusema, "Tazama Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake."

Yeye akasema, "Rabi, ulinijua lini?

214 Yeye alisema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona." Jamani!

215 Yeye alikuwa sehemu yake! Yeye alisema, "Wewe u Mwana wa Mungu! Wewe u Mfalme wa Israeli." Haijalishi jinsi ule—ule mdundo wa ulimwengu ulivyokuwa, na sherehe walizokuwa nazo za yale—yale madhehebu, hazikuwa ile Tarabu kuu ya Mungu. Amina. Yeye alisema, "Wewe ni Mfalme wa Israeli, Naam! Naiona. Naijua" Kwani? Yeye alikuwa amechaguliwa. Yule Mzao aliyechaguliwa ajua. Imekuwa hivyo kile wakati, kwamba wao wanajua.

216 Mwasema, "Lakini, Ndugu Branham, na mama yangu na baba je, na watu wangu, je, na dhehebu langu, je, na—nao watafanyaje? Watanifukuza. Sivyo . . . " Kama huwezi kutazama mbele, tazama juu. Usijaribu kutazama mbele, kwa vyovyote, weka mkono wako katika Wake. Mwache akuongoze. Tazama juu, usitazame mbele. Unasema, "Mbona, mbona wengine wananifanyia mzaha kuhusu nywele zangu ndefu, na kwa kutovalia suruali, na kuhusu kuondoka kwangu kanisani." Aha! Kuteswa kwa ajili ya Jina Lake, ni maumivu yanayoongezeka ya neema Yake. Naam. Kuteswa kwa ajili ya Neno Lake, mwaona, ni maumivu yanayoongezeka ya neema Yake. Naam, bwana! Kumbuka tu, ni neema ya Mungu ambayo umepewa. Lo Jamani!

217 Kama Paulo alivyosema, haleluya, yeye alikuwa na udhaifu, kitu fulani kilikuwa kikimuudhi. Yeye ali . . . Shetani ange—angemuudhi, pigo baada ya pigo. Naye alimsihi Bwana, mara tatu, akiondoe kwake, kasema, "Siutaki huu! Bwana, uondoshe kwangu!"

218 Ndiposa usiku mmoja Bwana akanena naye, akasema Sauli, au "Paulo, neema Yangu yakutosha."

219 Yeye alisema, "Basi nitajisifia udhaifu wangu. Nitajisifia kwake. Najua wewe u Mponyaji. Nimekuona Wewe ukiponya wagonjwa, ukifufua wafu, na kutoa pepo, ukiyafungua macho ya vipofu. Lakini ikiwa nimekusihi wewe, na unaniambia kuwa neema Yako yanitosha, basi huyu ibilisi anayeniudhi ni—ni maumivu yanayoongezeka ya neema Yako. Ndipo nitajisifia udhaifu wangu. Kwani? Makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi kwa wingi wa ufunuo huo." Mwaona?

220 Mnaona, yeye—yeye alikuwa na kitu fulani wanafunzi wale wengine hawakuwa nacho, alimwona Yesu baada ya kifo Chake, kuzikwa, kufufuka na kupaa. Alimwona Yeye. Wengine wao husema, "Vema, nilitembea pamoja Naye. "Vivyo hivyo, kila mtu barabarani. Lakini baada ya Yeye kufa, kuzikwa na kufufuka, na kupaa juu, na kurudi katika hali ya ile Nguzo ya Moto, Yeye alinena na Paulo. Hayo yalikuwa zaidi ya yote ye yote wao alikuwa nayo. Amina.

221 Yeye alisema, "Nisije nikajiinua juu sana na nitake kujenga seminari kuu na mengineyo, na mengine makubwa-makubwa, ili ni—nisijiinue kupita kiasi kwa wingi wa ufunuo huu, Mungu alimruhusu mjumbe wa Shetani aniudhi." Yeye alisema, "Basi niwapo mdhaifu, ndipo nina nguvu." Amina. Amina. Maumivu yanayozidi ya neema! Amina. Tungekaa kwa hilo kwa muda mrefu; saa moja na dakika arobaini na tano zimepita, na—na tunateseka kwa maumivu ya neema Yake.

222 Lo, Yeye aweza kuruhusu njia panda. Yeye aweza kuruhusu njia panda kutujaribu, zipate kutukamilisha sisi kwa utumishi Wake. Yeye aweza kuruhusu hilo sasa, Kanisa, hapa na pia hapo kwenye kanda. Yeye aweza kuruhusu njia panda kwa utumishi wetu.

223 Kama Yeye alivyomfanyia Danieli. Yeye alimpa Danieli njia panda dogo siku moja. Mwajua, yeye alikuwa mtu mkuu huko Babiloni. Alikuwa. Yeye aliruhusu, alifanya mfalme amchukie na kumtupa tunduni mwa simba. Hilo lilimkamilisha. Bila shaka!

224 Akaacha wana wa Waebrania waingie katika tanuru ya moto. Wao Waliamua kusimama kwa ajili ya Neno Lake!

225 Yeye aweza kuruhusu maneno makali, aruhusu kuchekelewa kwa kuwa na nywele ndefu, wakucheke kwa kusema umekuwa mtakatifu anayejigaragaza na kadhalika. Huenda wanaweza kukuruhusu ucheke. . . wanaweza kukuchekelea kwa ajili ya hilo, hilo, hilo, hivyo ni vema. Hiyo ni njia panda, hayo ni makutano madogo ya njia. Hilo ni kuthibitisha jambo fulani.

226 Mnaona, jambo pekee ambalo njia panda ilifanyia wale wana wa Waebrania waliosimama kwa Neno, ilikuwa kuwafungua kamba walizofungiwa nyayo na miguu yao.

227 Na wakati mwingine hapana budi kuwe na majaribu magumu kutufungua kamba za ulimwengu. Wakati mwingine Mungu huruhusu majaribu madogo, mwajua, kuona kile tutakachotenda, kukuondoa ulimwenguni. Ama, kwa maneno mengine, akuruhusu uwe na jaribu dogo na likuondoshe nje ya dhehebu hilo, na wazo hilo kwamba "Methodisti ndiyo pekee, Baptisti, au Pentekoste, au hilo—hilo ndilo kundi pekee walilo nalo. Usipoamini kama kanisa langu linavyoamini, hauamini hata kidogo." Wakati mwingine Yeye huruhusu jaribio dogo litokee. Labda una mtoto mgonjwa. Labda kitu fulani

kinatendeka wakati wa kufa. Labda mtu fulani ameondolewa kwako, au cho chote kile. Inafanya nini? Ni kukutenga wewe, kukwonyesha jambo fulani, kufungua macho yako. Labda unakuja kutoa lawama, wakati mwingine. Labda unasikiza ukanda huu kwa kutoa lawama tu. Labda Mungu anatenda hilo kuvunja baadhi ya kamba za kilimwengu zilizokufunga.

228 Kama mtu anayezama mtoni, yakupasa umtoe mtu huyo mtoni kabla hujatoa mto ndani yake. Naam. Yakupasa umtoe mtoni kwanza, kisha utoe mto ndani yake. Wakati mwingine yampasa Mungu afanye hivyo. Yeye huruhusu makutano, njia panda kufanya hivyo. Simama kwa ahadi Zake, lile Neno, maana hazikosi kutimia. Ya usoni yako mkononi Mwake. Simama kama walivyofanya, usi—usiondoke.

229 Ibrahimu, katika njia panda zake, alijua kuwa Mungu angemfufua mwanawe kutoka kwa wafu, kutoka ambapo yeye alimpokea kwenye njia panda. Ibrahimu alifika kwa njia yake panda. Na baada ya yeye kumtumainia Mungu na kuona miujiza yote ya Mungu. Kwa miaka ishirini na mitano Yeye alimngoja mwana wa kiume, mwana aliyeahidiwa, hatimaye Mungu akamwambia aende atoe sadaka kitu kile kile ambacho yeye alikuwa amekingoja. Loo, jamani, ni wakati wa jinsi gani! Lakini, je, Ibrahimu alitilia shaka? Soma warumi, sura ya 4, ilisema yeye alikuwa "akijua hakika." Amina. Yeye alijua hakika ya kuwa yale Mungu aliahidi, Mungu alikuwa aweza kuyatimiza. Amina. Yeye aliruhusu njia panda. Yeye alikuwa akituonyesha katika Ibrahim, mwaona, kuwa yu aweza kufufua wafu.

230 Ibrahimu alisema, "Nitampokea kama mmoja atokaye kwa wafu." Tumbo lake Sara lilikuwa limekufa, tumbo lake Sara lilikuwa limekufa; naye, mwili wake ulikuwa umekufa, pia alikuwa mzee. Yeye hakuwa na maziwa matitini mwake ya kumlisha mtoto wake mchanga. Na hakuwa na . . . Vema, hakukuwa na chochote. Naye alikuwa gumba, yeye binafsi, na Sara alikuwa tasa. Mwaona? Hakuna njia yo yote. Na yeye alimpokea kama mmoja aliyetoka kwa wafu, yeye alisema, "Ikiwa Mungu aweza kufanya hilo, Mungu aweza kumfufua toka kwa wafu. Maana Mungu yule yule aliyeniambia mwana angekuja, nami nilivumilia na akaja, Yeye aweza kumfufua toka kwa wafu." Maana, Yeye hufanya kila kitu kitende kazi na wale wampendao katika kuwapatia mema. Amina.

231 Mungu aliyetoa ahadi, katika siku zilizopita ya kwamba Mambo haya yangetendeka tunayoyaona yakitendeka: Ikiwa Yeye aliahidi mwana na mwana akaja; ikiwa Yeye aliahidi vitu hivi vyote tunvyoviona kote Maandikoni na vikatimia na tuingie katika mdundo wake. Yeye aliahidi katika siku za mwisho mambo haya yangetendeka, nasi twayaona. Yeye aliahidi kuwa angemtuma Yesu. Haleluya. Kutakuwa na ule Utawala wa Miaka Elfu. Kutakuwako na siku mpya, kutakuwako siku ambayo jua halitatua tena, kwa ile . . . hatutalihitaji tena, kwa kuwa yule

Mwana-Kondoo ndiye Nuru ya Mji huo ambamo tunaelekea. Amina.

232 Kumpambazuka kwa siku mpya, nakusikia mwilini mwote sasa. Ile Nuru ya siku mpya! Nuru ya siku ambapo hamna usiku, hamna giza, hamna vivuli, hamna anga, hamna utusitusi, anga nyeusi, hamna usiku wa manane, hamna makaburi, hamna maua kandoni mwa mlima, hamna sherehe za mazishi, hamna madaktari, hamna chumba cha maiti. Amina. Ni—ninaisikia ile—ile miali ya Nuru Yake ikiangaza juu ya nafsi yangu. Ile siku mpya! Ya kale inafifia.

233 Ninaposikia damu iharibikayo ikitiririka mwilini mwangu, nasikia ule mwinuko wa Roho Mtakatifu ukija nyuma yake, "Ondoka, na uangaze."

234 Kitu fulani kilisema, "Billy Branham, unakuwa mzee, unaanza kuwa dhaifu, mabega yako yainama, nywele zako zinageuka mvi na kung'oka." Naam. Ni giza na giza kuu juu ya nchi!

235 "Lakini ondoka, na uangaze!" Nasikia kushukiwa na msukosuko wa ile Nuru ya injili tukufu ya Yesu Kristo ambayo imenifanya mimi kiumbe kilicho hai katika Yeye. Natazamia siku hiyo, amina, siku mpya. Sijui ya usoni yalivyo. Sijui kile yanashikilia, mwaka huu wa 1964, unachoniwekea au cho chote kile, bali naushika mkono Wake Yeye ashikiliaye Milele, Aliye Milele. Amina.

236 Ibrahimu alijua kuwa Mungu angemfufua yeye tena, kwa hivyo alimtumainia.

237 Kwa hivyo, kwa mwaka mpya, jitahidi kudumu katika Neno Lake na kile limeahidi, kama wale wengine (Wateule) walivyofanya katika siku zilizopita. Ukijisikia kuwa umeona ile Nuru ambayo imekuangazia, ya Yesu Kristo, dhihirisho Lake la Roho Wake mkuu, aliye Mtakatifu, katika hizi siku za Mwisho. Na kumbuka, kumbuka, kaa nalo, Yeye alivyofanya, wewe u mmoja kati ya wale wateule; na kile huyo, Mteule katika siku zilizopita, kama Ibrahimu, Yeye alipoiona, wakati ilikuwa kinyume cha thibitisho la kisayansi. Nuhu aliiona, na yote ilikuwa kinyume cha thibitisho la sayansi. Musa aliiona, na yote ilikuwa kinyume cha thibitisho la sayansi. Hizi nyakati zenye elimu zilizopita; lakini wale wateule walioiona, walisimama imara! Amina.

238 Na kwa ya usoni, na tusimame imara kwa ahadi. Mungu aliahidi, ni juu ya Mungu kuitekeleza. Mimi naufuata mdundo tu. Inapodunda kumaliza wakati na kusema, "huu ndio mwisho wa William Branham duniani," ndipo nitakwenda na huo mdundo. Ndipo nitafufuka tena pamoja na mdundo huo. Haleluya. Yeye aliyeuanzisha, anaumaliza, tena anauanzisha. Ni mdundo wa Mungu, "Ninamfufua tena katika siku za mwisho. Yeye aniaminiye Mimi ana Uzima wa milele. Yeye asikiaye

Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka ana Uzima wa Milele; na hataingia hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani." Nitafuata mdundo wa Neno! Amina. Si mdundo wa moyo wangu. Mdundo wa Neno: Haijalishi jinsi lilivyo, moyo wangu usipodunda pamoja na Neno, basi moyo wangu umekosea. Amina. Maana, Yeye ni Neno! Amina. Biblia yatwambia hivyo, Mungu ni Neno.

239 Nilikuwa nasikiza kipindi cha redioni, kikitangazwa, Billy pamoja nami muda mfupi uliopita. Na ilikuwa ni Biblia hii . . . kile—kile kipindi kinachoitwa unabii, kile kipindi cha . . . Kinaitwaje? Kitu fulani kuhusu unabii. *Sauti ya Unabii*. Hakika, ni cha Seventh Day Adventist. Wamekuwa na majina mbalimbali manne au matano. Millerites, ndivyo walivyokuwa kwanza.

240 Wao ndio waliosema, hapo mkutanoni, kuwa "Nilidai eti mimi ni Yesu Kristo; kuwa Ba—Baba Mtakatifu alikuwa juu yangu, hiyo Nguzo ya Moto, na kwamba nilikuwa Yesu Kristo." Ikawa rafiki yangu alikuwa amesimama hapo kwenye huo mkutano wao mdogo, yeye akaamka na kusema, "Itakupasa uthibitishe hilo, kwa sababu nitamwita aje papa hapa. Nataka wewe uonyeshe wakati mmoja ambapo yeye alikiri hilo," waona, kama hivyo. Yeye alikuwa akinena kuhusu vikundi mbali mbali vya dini vilivyojitenga na mengineyo duniani.

241 Wao wanajua. Siku moja nilienda sare nao kuhusu hili swali la *Sabato*. Walishikilia siku ya kale iliyopita. Roho Mtakatifu ni Sabato yetu, Biblia ilisema hivyo, "Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, mizito nami nitawapeni sabato kwa nafsi zenu." Sio "siku." Paulo alisema, "Ninyi mnaoadhimisha siku nawaonea hofu." Mwaona, hiyo ni kweli. Ndio bwana. "Imesalia raha," Waebrania 4, "kwa watu wa Mungu, kuadhimisha sabato. Kwa maana sisi tulioingia katika raha hiyo, tumestarehe wenyewe katika kazi zetu, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake."

242 Lakini mtangazaji wao muda mchache uliopita, kipindi cha redioni kizuri, siwachukii. Ningefanya cho chote niwezacho kuwasaidia. Nawasamehe kwa kusema hayo, kwa sababu walisema kitu fulani ambacho hakikuwa kweli. Lakini haidhuru. Mafundisho yao yako tu kama ya Mashahidi wa Yehova na Christian Science na vikundi hivi vilivyojitenga vyote, mwaona, jambo lile lile. Lakini tazama, wao wako tu kama dhehebu lingine lo lote, wao hawajakosea zaidi, nadhani, ya wengine wao. Neno kila mara ni Kweli, mwaona, litajithibitisha lenyewe kabisa. Tazama.

243 Lakini yeye alipokuwa akiongea, mtu huyo alisema, "Tuna kitabu-cha-mwaka." Mwandishi huyu, loo, jina lake ni nani mtangazaji wake? Nasahau jina lake ni nani sasa. Yeye alinena kwa niamba ya Wafanyi Biashara Wakristo huko Seattle hapa muda mchache uliopita kwa Maonyesho ya Ulimwengu.

Na yeye—yeye alisema, huyu mtangazaji alisema, "Mtu huyu ameandika kitabu, kitabu kinachojulikana sana mwaka huu." Sikubaliani naye.

244 Kitabu cha mwaka huu ni Biblia! Ni Nuru ya ulimwengu. Ni Mungu Mwenyewe. Kitabu chetu cha Mwaka ni Biblia. Kwa mwaka wa 1964, kitabu chetu ni Biblia. Na miaka yote ijayo, Kitabu chetu ni Biblia. Miaka yote iliyopita, kimekuwa Kitabu cha miaka iliyopita, Kitabu cha miaka ijayo, na ni Kitabu cha Milele. Kinanjifunua kuwa ni Mungu. Naam, kinamfunua Mungu. Kila mwaka utakaokuja, ni Kitabu-cha-mwaka. Wakati—kila usikiapo Biblia ikinenea cho chote, ahadi yake imethibitishwa, kutakuwa Milele, siku moja. Biblia ndiyo itupayo ahadi hii, usikiapo Biblia ikisema kuwa siku yaja atakapokuja Yesu. Na kama ninavyosema leo hii . . .

245 Yanipasa nimalize sasa, kwa sababu ni—nimekuwa hapa kwa masaa mawili, mwaona, katika jambo lili hili.

246 Tazama, ikiwa—ikiwa Biblia yatwambia kuhusu mambo haya yatakayokuja, yanena kuhusu saa hizi zote ambazo—ambazo tumepitia. Zile siku za Nuhu zimetabiriwa. Zile siku za hawa wengine, Maandiko yalitabiri. Zile siku za Martin Luther, zilitabiriwa, zile siku za Wesley, zile siku za Pentekoste. Saa hii tunayoishi ilitabiriwa. Kila kitu kilitendeka tu hasa jinsi kilivyokuwa. Basi wakati . . . Ni nini? Neno lililonenwa la Mungu, ambalo limethibitishwa na Mungu, linaifanya Nuru ya wakati huu. Mwaona, kama tu jua lilivyo. Wakati Neno, Neno lenyewe, ni Nuru linapothibitishwa ya ule wakati ulio wake. Mwaona, likithibitishwa, basi ni Nuru ya wakati.

247 Yohana alikuwa ile Nuru, yeye—yeye alikuwa na Nuru zaidi kuliko Eliya na hao wengine walivyokuwa nayo. Eliya. Yeye hakuwa Nuru ya Eliya, lakini yeye alikuwa Eliya kwa hali nyingine, a—akithibitisha Nuru. Mwaona, alikuwa hivyo. Na Yesu alipokuja, Yeye alisema, "Yeye alikuwa taa iwakayo na kung'aa kwa muda. Nanyi mlipenda kuishangilia nuru Yake." Mwaona?

248 Naye Yohana alisema, "Sasa ni lazima nififie. Lazima niondoke sasa, Nuru yangu imemaliza kuangaza. Ni lazima niondoke. Hana budi kuongezeka. Yeye ndiye Nuru."

249 Yeye alisema, "Mimi ni Nuru ya ulimwengu." Amina. Naam. "Ni Yeye Yule jana leo, na hata milele." Na Yeye yuangali Nuru ya ulimwengu. Na Yeye yu nini? "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu." Kwa nini Yeye alikuwa Nuru ya ulimwengu? Ikiwa Yeye angekuja, kasema Yeye alikuwa Masihi, na asitende jinsi Biblia ilisema Masihi angetenda, basi Yeye hangekuwa Nuru ya ulimwengu. Mwaona, ni Neno lililothibitishwa ambalo linaifanya Nuru ya ulimwengu.

250 Na katika wakati huu tunaoishi sasa, Neno lililothibitishwa la wakati huu! Wapentekoste, mwasema, "kunena kwa lugha,"

na mengineyo. Hiyo ilikuwa siku ya Pentekoste, hiyo ilikuwa Nuru ya wakati huo basi. Mwaona? Hii ni siku nyingine. Yeye ndiye Nuru ya wakati huu leo.

251 Ule Wakati wa Kanisa wa Saba, wote umefunikwa, Kristo akiwa nje. Mwezi unatambulisha, giza lote likija juu ya nchi. Nuru inajisukumiza ndani sasa, inaanza kuonyesha kile kitakachotendeka. Kitu hicho kitaangamizwa na Nuru itaingia na kukiangamiza. Na watakatifu watairidhi nchi. Wapole watairidhi nchi. Nchi, lile giza la mwezi litaondolewa. Lile giza la usiku litakwisha, giza pamoja na vifo vyake na kanuni zake za imani, na mambo yaliyo mbali na Neno la Mungu, mambo yaliyopotoshwa wanayoyasema. Nayo Nuru itajitokeza siku hiyo.

252 Basi kumbuka, wakati Bibla nzima...Sikiza, katika kufunga. Wakati Biblia nzima imekwisha kuthibitishwa kabisa, ndipo kutakuwako na Shalom ya Milele, Amani ya Milele. Mwaona?

253 Yeye alikuja na kusema alikuwa, "Amani duniani, kwa watu aliowaridhia," lakini ulimwengu haukuipokea. Mwaona? Yeye alikuwa Amani kwa kila mmoja aliyemjia kwa ajili ya Amani. Mwaona? Amani duniani, kwa watu aliowaridhia, Yeye alikuwa Amani ya mwanzo wa mwaka huo mpya, siku mpya ya Mungu. Kwa nini? Yeye alikuwa Nuru iliyothibitishwa ya siku hiyo. Mwaona?

254 Lakini kuna Neno zaidi litakalothibitishwa. Yeye hana budi athibitishe Neno zaidi. Na Neno la mwisho linapothibitishwa, namaanisha, litakapodhibitishwa, ndipo mauti itakapomezwa kwa kushinda, nao wafu katika Kristo watafufuka, ule Utawala wa Miaka Elfu utaanza; na itakuwa Amani moja kuu, Shalom. Tuiishie siku hiyo, ndugu, dada, kwenye Shalom hiyo moja kuu.

255 Kumbuka, Biblia ndiyo msingi wa hekima yote na inashikilia tumaini zote za usoni. Kwa kanisa, Shalom! Na tuombe.

256 Kundi dogo lililoko hapa sasa. Ni—nimekuwa hapa kwa masaa mawili juu—juu ya Ujumbe mdogo wa mwaka mpya. Mmekuwa na subira sana. Kunaye mmoja ndani hapa asubuhi hii, au—au, namaanisha, jioni hii, asiye na Shalom hiyo, Amani iliyonena, hilo neno lililotambulishwa la Mungu wakati wewe na Neno mlikuwa mmoja? Ambapo, ikiwa Biblia inaposema kitu kimoja, nawe wasema "la, ni vigumu kwangu kuamini kuwa hilo ni kweli," basi huna Shalom. Huna Amina na Mungu, kwa sababu Neno lasema Jambo moja nawe haukubaliani Nalo.

257 Na ikiwa Neno lasema, "Shalom, Amani," nawe una Amani hiyo, hata kila Neno asemalo Mungu waweza kuliitikia na "amina", nawe unaliamini. Na uonapo likithibitishwa, unasema, "Amina, hilo ni Neno!" Lakini, je, kanuni ya imani, nuru, nuru ya uongo, ulimwengu unaenenda katika kivuli cha nuru ambayo inaonyeshwa ili kuitia giza, kanuni fulani za imani, kusema, "La,

ni—ninadhani kuwa—kuwa Hilo lilikuwa kwa kitu kingine. Hilo halimaanishi hayo kamwe," na bado Neno linasema hayo? Je, unakifuata kivuli hicho, au unatokea pamoja na hiyo Nuru?

258 Hapa na kwenye kanda, ye yote atakayesikia, waza kuyahusu kwa muda mfupi. Na kukiwa mmoja aliye hapa ambaye angependa, ambaye hana Nuru hiyo, mbona usiuinue mkono wako kujitambulisha mwenyewe, kuwa uko tayari kutembea katika Nuru hiyo leo. Na ikiwa kunaye mmoja nje mahali fulani ambapo kanda hii itakwenda, ikiwa hauna, na uinue mkono wako kwa Mungu papo ambapo . . . Zima chombo chako cha kunasia sauti kwa muda mfupi tunapoomba, piga magoti yako, na kusema, "Bwana Mungu, nimeshuku ni—nimetenda hili. Nimewaza, "Vema, kwa Sababu kanisa lilisema mambo hayo hayangekuwa, na hili halingekuwa." Ingawaje, lakini naona limeahidiwa katika Biblia, na naona mambo mengi sana. Hata na mbingu ziliyatangaza, zenyewe. Na mambo haya yanayosemwa, yatendeka vivyo hivyo. Na Mungu aliye Mbinguni anatangaza jambo lile lile. Kwa hivyo nataka kulipokea sasa. Na Neno la Mungu liingie ndani yangu. Hebu na—nami niingie katika huo mdundo wa kutosikiza yale kanisa au mhubiri anayosema; lakini hebu niingie katika mdundo wa Neno, na kuona kile lisemacho, na hebu linilete, katika hii Tarabu ya Mungu, kudunda kwa mapenzi Yake maishani mwangu."

259 Baba yetu uliye Mbinguni, sasa twakuletea Wewe kila mkono ulioinuliwa kila mahali. Na ruhusu Roho Mtakatifu wa Mungu awaletee ule mdundo wa Neno na Kweli Yake, ya kwamba wao hawana budi kuundwa sasa kuwa wana wa kiume na wa kike wa Mungu, na watakuwa onyesho la nuru ya Mungu hapa duniani. Yapasa wawe Neno lililodhihirishwa, kwamba waume kwa wake wataishi kama kila Neno la Mungu na kuishi kwalo kama Yeye alivyofanya, maana Yeye alisema, "Mwanadamu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu." Si Maneno macheche tu, sehemu ya Maneno, bali "Kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu!

260 Neno la wakati wa Musa halikufanya kazi katika siku za wakati wa Yesu. Neno, lile Neno katika siku za mitume halifanyi kazi katika siku hizi. Ni neno lililoahidiwa kwa siku hii. Walilinena wenyewe, wakalinena kwa Roho Mtakatifu, yale yangetendeka katika siku za mwisho, jinsi makanisa yangekuwa makaidi, wenye kujivuna, jinsi yule kahaba angeinuka nao makahaba waambatane naye, na jinsi wangeitia giza duniani. Na katika wakati wa mwisho wa kanisa, Laodikia, Yesu ataondolewa kabisa kanisani.

261 Ewe Bwana, na nikae pamoja Naye, yule Neno. Na nidhihirishe Nuru Yake, kupitia kwetu sote, tunapoingia katika huu mwaka mpya tukiwa na juhudi. Hatujui kile mwaka huu mpya unachoshikilia, lakini tunajishikilia Kwake, yule Neno, ajuaye hiyo Tarabu tangu mwanzo hata mwisho. Yeye ajua kila

hatua na kila makutano. Na, Bwana tunamtazama Yeye tu, tukimkazia macho yetu, yule Neno. Kisha tuonapo haya yakija, tunajua tuko ndani ya mdundo wa Neno. Tujalie. Okoa kila nafsi iliyopotea, Bwana, iliyo hapa, na kila mmoja asikiaye ukanda huu. Tunawakabidhi Kwako, kwa ajili ya ufalme Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Shalom SWA64-0112
(Shalom)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Januari 12, 1964, kule Sierra Vista, Arizona, Amerika, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org